# VITENDO SOGEZI KATIKA KISWAHILI SANIFU

Na

EDWIN OCHIENG' MUNA

C50/82890/2015

Tasnifu hii imewasilishwa kwa ajili ya kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Nairobi.

IDARA YA KISWAHILI

CHUO KIKUU CHA NAIROBI

JULAI 2017

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe. Haijawahi kuwasilishwa katika chuo kikuu chochote kile kwa ajili ya kutimiza mahitaji ya shahada yoyote ile.

Edwin Ochieng' Muna

Sahihi Tarehe...................................

## IDHINI

Tasnifu hii imewasilishwa kwa minajili ya kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi tulioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

Dkt. Prisca Jerono

Sahihi........................................................ Tarehe......................................

Bw. B.G. Mungania

Sahihi......................................................... Tarehe........................................

**TABARUKU**

Kazi hii ninamtabarukia MUNGU MKUU WA ISRAELI, MUNGU WA NABII MKUU WA MUNGU, aliyekiumba Kiswahili kwa ustadi wa kuajabisha. Moyo wangu unakupa sifa na utukufu wote unaostahili.

**SHUKRANI**

Kwanza kabisa, ninamshukuru MUNGU MTAKATIFU WA ISRAELI kwa kunipa uhai, uzima na fursa ya kuendeleza masomo yangu hadi kiwango hiki. Bila MUNGU singeweza kupata mafanikio haya hata siku moja. Ninamshukuru sana NABII MKUU WA BWANA kwa kuwa kibali cha kurudi chuoni nilikipata baada ya MAOMBI YAKO. Pia, ninamshukuru Askofu wangu Julius Kimani kwa maombi yake ya kila mara ambayo yamechangia pakubwa katika safari hii ya masomo.

Pili, ninamshukuru mke wangu mpendwa Maximilla Muna kwa mapenzi makuu na uvumilivu mkubwa ulioshamiri moyoni mwako kwa wakati huu niliozamia vitabu na madarasa. Ninakushukuru kwa himizo zako za kila siku. Wewe ni msaidizi wangu wa dhati. Ufanifu huu ni wetu sote.

Uandishi na ukamilifu wa tasnifu hii haingefanikiwa kamwe bila msaada na ushauri wa busara wa wasimamizi wangu Dkt. P. Jerono na Bw. B.G. Mungania. Ninawashukuru sana kwa juhudi zenu mlizowekeza kufanikisha utafiti huu. Moyo wangu unawashukuru hadi ya kushukuru. Alama za ushauri wenu zimehanikiza katika tasnifu hii kuanzia ukurasa wa kwanza hadi wa mwisho. MUNGU awabariki sana.

Ninashukuru Chuo Kikuu cha Nairobi kwa kufadhili masomo yangu ya uzamili na hata kunipa fursa adimu ya kusomea Chuo Kikuu cha Humboldt cha Berlin kwa muhula mmoja. Msaada wenu umekuwa wa natija kubwa kwangu. Fauka ya hayo, ninakishukuru Chuo Kikuu cha Humboldt kwa kunifadhili kusomea Ujerumani kwa muhula mmoja. Vitabu na makala nilizozipata maktabani mwenu zilichangia pakubwa katika uandishi wa tasnifu hii.

Vilevile, ninawashukuru wahadhiri wangu wote wa thamani katika Chuo Kikuu cha Nairobi: Prof. Iribe Mwangi, Prof. Abdulaziz, Prof. Mbatia, Prof. wa Mutiso, Prof. Habwe, Prof. Rayyah, Dkt. Zaja, Dkt. Olali, Dkt. Mwaliwa, Dkt. Mbuthia, Dkt. Mukhwana na Dkt. Buregeya. Ninawashukuru sana kwa kuunganisha mikono yenu pamoja kunifinyanga kielimu. Ninawahakikishia kuwa juhudi zenu hazijaenda pewa hata kidogo. Mradi umefanikiwa pakubwa. Siwezi kuwasahau wahadhiri wangu katika Chuo Kikuu cha Humboldt Berlin: Prof. Gueldemann, Dkt. Lutz na Dkt. Neumann. Asanteni kwa ushauri wenu.

Wengine ninaowashukuru ni pamoja na mwalimu mkuu wa Shule ya Upili ya Brucewood Nairobi Dkt. J. Kimani na walimu wote wa shule hiyo kwa kila msaada mlionipa wakati wa masomo yangu. Pia ninamshukuru kakangu mlungizi Tyson kwa upendo na himizo alizonipa wakati wa masomo yangu.

Siwezi kuwasahau wanafunzi wenzangu tuliosaidiana na kuhimizana nao katika mchakato huu wa kuchimba zaidi katika migodi ya elimu ya chuo kikuu. Asanteni sana Ngulamu Mwaviro, Albert Otwera, Zipporah Kitiku, Purity Kolongei, Lilian Chacha na Joshua Anusu. Sote tumeibuka na kito bongoni na mikononi. MUNGU awabariki.

## IKISIRI

Katika miaka ya tangu 1970, watafiti mbalimbali wamechunguza uanisho wa lugha za ulimwengu uliofanywa na Talmy (1975, 1985, 2000) kwa kuzingatia vitendo sogezi. Talmy anaeleza kuwa kitendo sogezi kina vipengele vinne vya ndani na lazima na vipengele viwili vya nje na hiari. Anatumia kipengele cha njia kuainisha lugha za ulimwengu katika aina mbili: mfumbatio-tenzi na mfumbatio-kifuatilizi kwa kutegemea kipashio cha kileksia au kisintaksia kinachoeleza kipengele hiki cha kisemantiki. Kumekuwapo na madai kuwa lugha zote za Kiafrika, ikiwamo Kiswahili, ni lugha za mfumbatio-tenzi (Taz. Schaefer & Gaines 1997, Fortis 2010). Hata hivyo, madai haya yametolewa bila utafiti wa kuridhisha kuhusu vitendo sogezi katika Kiswahili. Katika utafiti huu, hivyo basi, nililenga kubainisha uainisho muafaka kwa lugha ya Kiswahili kuhusiana na vitendo sogezi na vipashio vinavyotumika kueleza vipengele vya vitendo sogezi katika lugha hii na vipashio ambavyo huleksisha vipengele vya vitendo sogezi. Ili kufikia malengo haya, nilikusanya data kwa majaribio mawili. Katika Jaribio la 1 washiriki walipewa vitenzi kadha vya usogezi ili wavitungie sentensi. Katika Jaribio la 2 washiriki walipewa kitabu cha picha cha Mayer (1969) na kuombwa kusimulia matukio yaliyomo katika kila ukurasa. Nilichanganua data kwa kuzingatia mawazo ta Talmy aliyoyapendekeza kwa misingi ya nadharia ya Semantiki Tambuzi. Nilibainisha kuwa, ingawa Kiswahili hueleza kipengele cha njia katika vifuatilizi, hupendelea zaidi kuleksisha kipengele hiki katika mizizi ya vitenzi sogezi vyake. Kwa hivyo, Kiswahili ni lugha mfumbatio-tenzi. Vilevile, nilibainisha kuwa Kiswahili hutumia vipashio kama viambishi, maneno, virai na vishazi kueleza vipengele mbalimbali vya vitendo sogezi.

**VIFUPISHO NA ISHARA**

| | |
|---|---|
| KE- | Kirai Elezi |
| Kf- | Kifuatilizi |
| KN- | Kirai Nomino |
| KH- | Kirai husishi |
| L- | Lengo |
| M- | Msingi |
| Mw- | Mwelekeo |
| n.w- | na wengine |
| T- | Kitenzi |
| TY- | Tafsiri yetu |
| Taz.- | Tazama |
| U- | Umbo |
| X- | kipashio cha kisarufi |
| ≠- | si |

**YALIYOMO**

Ungamo........................................................................................ii
Idhini............................................................................................ii
Tabaruku.....................................................................................iii
Shukrani.....................................................................................iv
Ikisiri...........................................................................................v
Vifupisho....................................................................................vi

**SURA YA KWANZA**

1.0 Usuli wa mada..........................................................................1
1.1 Utangulizi....................................................................................1
1.2 Tatizo la utafiti............................................................................3
1.3 Maswali ya utafiti.........................................................................4
1.4 Malengo ya utafiti.........................................................................5
1.5 Umuhimu wa utafiti......................................................................5
1.6 Upeo wa utafiti.............................................................................6
1.7 Msingi wa Nadharia......................................................................6
1.7.1 Nadharia ya Semantiki tambuzi...............................................7
1.7.2 Mifumo ya Urejelezi.................................................................12
1.7.2.1 Mfumo wa urejelezi sahili......................................................14
1.7.2.2 Mfumo wa urejelezi halisi......................................................14
1.7.2.3 Mfumo wa urejelezi husishi....................................................14
1.8 Yaliyoandikwa kuhusu mada.......................................................15
1.8.1 Maandishi kuhusu vipashio vya Kiswahili.................................15
1.8.2 Maandishi kuhusu vitendo sogezi..............................................16
1.9 Mbinu za Utafiti...........................................................................20
1.9.1 Jaribio la 1..................................................................................20
1.9.2 Jaribio la 2..................................................................................21

**SURA YA PILI**

2.0 Vipengele vya vitendo sogezi........................................................23
2.1 Utangulizi......................................................................................23
2.2 Maelezo.........................................................................................23
2.2.1 Usogezi........................................................................................25
2.2.2 Umbo...........................................................................................26
2.2.3 Chanzo.........................................................................................29
2.2.3.1 Maelezo ya chanzo kwa KH.....................................................30
2.2.3.2 Maelezo ya chanzo kwa kielezi au KE......................................30

2.2.3.3 Maelezo ya chanzo kwa Kishazi kitegemezi............................30
2.2.4 Lengo..........................................................................30
2.2.4.1 Maelezo ya lengo kwa Nomino na KN....................................31
2.2.4.2 Maelezo ya lengo kwa Kielezi na KE......................................31
2.2.4.3 Maelezo ya lengo kwa kishazi ktegemezi.................................32
2.2.5 Msingi-pitwa.................................................................32
2.2.6 Kisababishi..................................................................32
2.3 Vitenzi vya usogezi.........................................................33
2.3.1 Sifa za vitenzi vya usogezi..........................................34
2.3.2 Aina za vitenzi vya usogezi..........................................36
2.3.2.1 Vitenzi vya usogezi unaoelekezwa...........................................37
2.3.2.2 Vitenzi vya namna ya usogezi..................................................37
2.3.2.3 Vitenzi vya namna ya usogezi kwa chombo.............................38
2.3.2.4 Vitenzi vya usababishi.............................................................38
2.3.2.5 Vitenzi vya kuandama.............................................................40
2.3.2.6 Vitenzi vya mpitano.................................................................40
2.4 Muhtasari.........................................................................41

**SURA YA TATU**

3.0 Maelezo ya namna katika Kiswahili sanifu......................................42
3.1 Utangulizi..........................................................................42
3.2 Maelezo............................................................................42
3.2.1 Namna katika vitenzi........................................................42
3.2.1.1 Vitenzi vya usogezi vya namna ya kasi.......................................43
3.2.1.2 Vitenzi vya usogezi vya namna ya mtindo wa usogezi...............44
3.2.1.3 Vitenzi vya usogezi vya namna ya urudiaji.................................44
3.2.1.4 Vitenzi vya usogezi vy namna ya kuingia katika lengo...............45
3.2.1.5 Vitenzi vya usogezi vya namna ya kutoka katika chanzo............46
3.2.2 Uleksishaji wa namna katika vifuatilizi..........................................46
3.2.2.1 Kielezi na KH.......................................................................46
3.2.2.1.1 Kasi ya usogezi wa umbo........................................................47
3.2.2.1.2 Mtindo wa usogezi wa umbo....................................................47
3.2.2.2 Namna katika Kishazi kitegemezi.................................................48
3.2.2.2.1 Vitenzi viwili vya namna...........................................................48
3.2.2.2.2 Kitenzi cha njia na kitenzi cha namna........................................49
3.2.2.3 Viigizi...........................................................................49
3.2.2.3.1 Kiigizi katika chanzo................................................................49

3.2.2.3.2 Kiigizi katika lengo....................................................................49
3.2.2.3.3 Kiigizi katika msingi-pitwa.........................................................50
3.2.2.3.4 Kiigizi katika njia........................................................................50
3.2.2.4 Kirai husishi....................................................................................50
3.2.2.4.1 Chombo cha usogezi...................................................................51
3.2.2.4.2 Hisia inayoandamana na kitendo sogezi.....................................51
3.2.2.4.3 Nguvu au msukumo uliotumiwa katika usogezi..........................51
3.2.2.4.4 Namna ya kasi ya usogezi wa umbo...........................................52
3.2.2.5 Maelezo ya namna kwa tashbihi....................................................52
3.2.2.5.1 Tashbihi zinazoonyesha kasi ya usogezi.....................................53
3.2.2.5.2 Tashbihi zinazoonyesha mtindo wa usogezi...............................53
3.2.2.6 Namna isiyokuwepo........................................................................53
3.3 Muhtasari...........................................................................................54

**SURA YA NNE**

4.0 Maelezo ya njia katika Kiswahili sanifu..............................................55
4.1 Utangulizi...........................................................................................55
4.2 Maelezo..............................................................................................55
4.2.1 Aina za njia za usogezi.......................................................................56
4.2.1.1 Njia funge.........................................................................................56
4.2.1.2 Njia za mwelekeo.............................................................................57
4.2.1.3 Njia za mapitio..................................................................................58
4.2.2 Njia katika vitenzi...............................................................................59
4.2.2.1 Vitenzi vya njia funge.......................................................................61
4.2.2.2 Vitenzi vya njia ya mapitio...............................................................62
4.2.2.3 Vitenzi vya njia ya mwelekeo...........................................................63
4.2.3 Njia katika vifuatilizi...........................................................................63
4.2.3.1 Njia katika kihusishi au KH...............................................................63
4.2.3.1.1 Njia funge.......................................................................................63
4.2.3.1.2 Njia za mwelekeo...........................................................................64
4.2.3.1.3 Njia za mapitio................................................................................64
4.3 Mifumo ya urejelezi na njia za usogezi.................................................64
4.3.1 Mfumo wa urejelezi sahili....................................................................65
4.3.2 Mfumo wa urejelezi husishi..................................................................65
4.3.3 Mfumo wa urejelezi halisi....................................................................68
4.4 Muhtasari.............................................................................................68

**SURA YA TANO**

5.0 Matokeo ya Utafiti na Hitimisho........................................................69
5.1 Utangulizi........................................................................................69
5.2 Matokeo ya utafiti.............................................................................69
5.3 Hitimisho..........................................................................................71
MAREJELEO.........................................................................................72

**ORODHA YA MICHORO**

Mchoro 1...............................................................................................45
Mchoro 2...............................................................................................58

**ORODHA YA JEDWALI**

Jedwali 1...............................................................................................69

# SURA YA KWANZA

## 1.0 USULI WA MADA

### 1.1 UTANGULIZI

Kuanzia miaka ya 1970, dhana ya vitendo sogezi imeshughulikiwa na wanaisimu tofauti tofauti kwa njia mbalimbali. Ilivyo ni kuwa dhana ya usogezi ni mojawapo ya dhana ambazo ni vigumu kuzitolea fasili kwa maneno katika lugha. Hali hii huenda inatokana na dhana hii kuwa inahusu utambuzi wa binadamu na kwamba si kitu kinachogusika kwa mikono au kuonekana kwa macho. Katika tasnifu hii, ninavifasili vitendo sogezi kama vitendo vinavyohusu kusonga kwa kitu kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa mpito wa wakati. Vilevile, wapo wataalamu ambao wamejaribu kuifasili dhana hii kwa namna mbalimbali. Kulingana na Rudzka-Osty (1988:517) anayenukuliwa na Filipovic' (2007), "Kimsingi, usogezi si kitu chochote ila mfuatano wa mabadiliko ya mahali palipo kati ya kitu na mawanda yake." (TY). Kwa hivyo, maelezo yake yanasisitiza vipengele vya vitendo sogezi vinavyohusiana na badiliko la mahali ambapo kitu kipo.

Ikegami (1990:87) ambaye pia ananukuliwa na Filipovic' (keshatajwa) anaeleza kuwa, "Vitenzi vya usogezi hueleweka...kama vile ambavyo hueleza badiliko la mahali." (TY) Kwa hivyo hata naye anasisitiza kuwa vitendo sogezi huhusisha badiliko fulani la mahali ambapo kitu kipo. Miller (1973:338) ambaye pia anatajwa na Filipovic' anaeleza kuwa:

> [...] ni sharti lugha iwe na akiba kubwa ya maneno ya kueleza namna kitu kilicho katika mahali M1 [mahali kabla ya usogezi] wakati W1 [wakati wa kuanza kwa usogezi] kinakuja kuwa katika mahali M2 [mahali baada ya usogezi] wakati mwingine unaofuatia W2 [wakati wa kuhitimika kwa usogezi]. TY

Japo maelezo haya yanatofautiana kwa namna moja ua nyingine, ni wazi kuwa walioyapendekeza yanasisitiza kuwa katika usogezi lazima kuwe na badiliko fulani la mahali kitu kilikuwa kabla ya usogezi hadi mahali pengine baada ya usogezi na kuwa badiliko hilo hutendeka kwa muda fulani. Vile vile, kila lugha lazima iwe na uwezo wa kueleza vitendo sogezi kwa sababu hakuna jamii isiyokuwa na vitendo sogezi. Kwa hivyo, ni sharti lugha iwe na vipashio au maneno yafaayo kutimiza wajibu huu. Sharti

kila lugha iwe na uwezo wa kueleza vitendo sogezi katika leksikoni yake. Hivyo basi, ni wazi kuwa vitendo sogezi huelezwa kwa kutumia lugha, yaani huleksishwa humo.

Kwa upande wake, Talmy (1985:85) anaeleza matukio ya usogezi kama, "hali zinazoonyesha kusonga au kutuwama katika sehemu moja." Kwa hivyo, kulingana naye, usogezi huhusu kutoka sehemu moja hadi nyingine au kusalia katika sehemu moja tu. Talmy anashikilia kuwa kitu kinaweza kusonga kutoka sehemu moja hadi nyingine au kikasonga palepale kilipo bila kutoka hapo. Matlock et al (2011) wanatambua aina tatu za usogezi: usogezi halisi, usogezi bunifu na usogezi dhahania. Usogezi halisi ni ule usogezi unaohusu vitu halisi na kuwa kitu kimoja kinatoka sehemu moja hadi nyingine na athari ya usogezi huo inaweza kuonekana. Wanaeleza usogezi bunifu kama usogezi usiokuwa halisi na unaorejelewa kwa sentensi kama *Barabara ile inapitia jangwani*. Vilevile, wanamnukuu Langacker (1986, 1987) ambaye anaeleza kuwa usogezi dhahania huhusika katika kuhesabu, kukariri abjadi na uchakataji akilini wa vitu vinavyofuatana. Hoja hapa ni kuwa watu husonga kutoka kwa ishara moja hadi nyingine katika akili zao wanapochakata ishara zinazofuatana akilini mwao.

Wataalamu mbalimbali wamedai kuwa uelewa wetu wa dhana ya vitendo sogezi hujengwa kwa mfumo ishara wa ubia (unaopatikana ulimwenguni kote). Hata hivyo, lugha mbalimbali hudhihirisha tofauti wazi kuhusu namna vipengele vyake tofautitofauti vya kisemantiki vinavyoleksishwa. Talmy (1985, 1991) alishughulikia uhusiano uliopo kati ya umbo na maana katika uwanda wa usogezi huku akilinganisha lugha mbalimbali. Aligundua kuwa lugha hutofautiana kwa namna ambavyo vijenzi vya kisemantiki vya vitendo sogezi vinavyoelezwa kwa kutumia vipashio dhahiri vya lugha. Kwa kutegemea mfumo wa uleksishaji alizokumbana nazo, Talmy alipendekeza mfumo wa uanishaji ambao unazingatia ruwaza ya kudhihirisha vitendo sogezi katika lugha mbalimbali. Uleksishaji ni namna ambavyo tunayoyapitia yanaelezwa katika lugha kwa kutumia maana zilizomo katika vipashio vya kileksia. Ni namna ya upakiaji wa maana zilizomo akilini katika vipashio vya kileksia.

Jambo lililo wazi hapa ni kuwa vitendo sogezi huelezwa kwa namna mbalimbali na kwa vipashio tofautitofauti katika lugha za ulimwengu. Dhana hii imefanyiwa tafiti

mbalimbali na wataalamu tofautitofauti kama vile wanaisimu, wanasaikolojia, wataalamu wa ubongo na wanafalsafa. Tulivyotaja hapo juu, matokeo ya tafiti za awali yanadhihirisha kuwa yumkini kila lugha hueleza dhana hizi kwa namna yake maalumu. Baadhi ya wataalamu ambao wamezishughulikia dhana hii katika lugha mbalimbali, kwa mitazamo tofautitofauti na kwa malengo anuwai ni kama vile Talmy (1972, 1975, 1985, 1991, 2000, 2007), Slobin (1996, 2000, 2004), Ameka & Essegbey (2013), Chen & Guo (2009) na wengine wengineo. Tafiti zao zimetoa mchango mkubwa katika uelewa wa dhana hii na hata kuchochea utafiti zaidi kuihusu. Yapo maswala ambayo bado yanazua mjadala na utata katika utafiti wa dhana ya vitendo sogezi. Chanzo kimoja cha utata uliomo ni madai ya awali ya Talmy kuhusu kuwepo kwa lugha ambazo zinaeleza njia katika vitenzi na zile ambazo zinaeleza njia katika vipashio vingine vinavyofuata vitenzi vilivyomo katika sentensi. Katika utafiti huu, nitairejelea aina hiyo ya kwanza ya lugha kama lugha mfumbatio-tenzi huku aina hiyo ya pili tukiita lugha mfumbatio-kifuatilizi. Kifuatilizi hapa ninakitumia kurejelea dhana ambayo Talmy aliita "Satellite". Talmy (1991:486) anakifasili kifuatilizi kama "...kipashio cha kisarufi ambacho si nomino na kipo katika uhusiano wa kidada na kitenzi husika" (TY). Hata hivyo, kulingana na fasili hii ya Talmy, kifuatilizi husika huwa katika kishazi kimoja na kitenzi kinachohusiana nacho. Watafiti kadha wametoa maoni yao kuhusu huu uainishaji wa Talmy. Kuna wale ambao wameutilia shaka kama vile Ameka & Essegbey (keshatajwa) huku wengine kama Slobin (2004) wakiuunga mkono na hata kupendekeza upanuzi wake.

## 1.2 TATIZO LA UTAFITI

Ni kweli kuwa tafiti zimefanywa kwa wingi kuhusu vitendo sogezi katika lugha mbalimbali duniani. Hata hivyo, ni dhahiri kuwa tafiti hizo za awali zimefanywa kwa upendeleo wa lugha fulani fulani duniani. Baadhi ya tafiti hizo zimefanywa kuhusu lugha za Kihindi-Uropa kama vile Kigiriki, Kilatini, Kiingereza, Kijerumani au Kirusi. Huu si mwelekeo mwema kwa kuwa vitendo sogezi, tulivyotaja awali, hupatikana katika lugha zote za ulimwengu na kuwa, inavyodaiwa na wataalamu kadha, huelezwa kwa njia zilizo tofauti katika kila lugha au jamii ya lugha. Huenda hali hii imetokana na hali kuwa baadhi ya watafiti wa awali walitoka katika maeneo ambako lugha nilizozitaja hapo juu zinazungumzwa.

Ingawa kuna tafiti zilizofanywa kuhusu lugha fulani za Afrika Magharibi na Kusini, ni wazi kuwa lugha nyingi za Kiafrika zimepuuzwa katika tafiti hizo. Ni hivi karibuni tu ambapo watafiti wameanza kuangazia maelezo ya vitendo sogezi katika lugha za Kiafrika. Kwa mfano, Ameka na Essegbey (keshatajwa) wanafanya utafiti kuhusu vitendo sogezi katika lugha za Ewe na Akan. Jerono (2017) anashughulikia vitendo sogezi katika lugha ya Tugen inayozungumzwa katika Bonde la Ufa nchini Kenya.

Wataalamu husika wamezipuuza lugha kama Kiswahili, labda kimakusudi, kwa kuchukulia kuwa tafiti zilizofanywa katika lugha nyingine zingetosha kudhihirisha maelezo ya vitendo sogezi katika Kiswahili na lugha nyingine zilizosalia au kuwa kutotafitiwa huko kumetokea tu kwa bahati mbaya. Jambo la kushangaza, hata hivyo, na ambalo ndilo tatizo la utafiti huu, ni kuwa Fortis (2010) anaorodhesha Kiswahili kama lugha ambayo inatumia mfumo wa mfumbatio-tenzi. Ninaona kuwa dai hili lilitolewa bila kufanya utafiti wa kina kuhusu lugha yenyewe. Je, madai ya Fortis yana mashiko yoyote? Vilevile, Schaefer na Gaines (1997), baada ya kufanya utafiti wao kuhusu lugha za Kinaija na Kikordofani, wanatoa madai ya jumla ambayo yanazua utata kuwa lugha zote za Kiafrika (na kwa hivyo hata Kiswahili) ni lugha zinazoleksisha njia katika vitenzi. Hii hatua yao ya kujumuisha lugha zote za Kiafrika katika kundi la lugha za mfumbatio-tenzi, kwa maoni yangu, imechukuliwa haraka tena bila utafiti wa kutosha. Kwa maoni yangu, uamuzi wa kuiainisha lugha kama ni ya mfumbatio-tenzi au mfumbatio-kifuatilizi unapaswa kuafikiwa tu baada ya kufanya utafiti wa kuridhisha katika lugha husika. Hali kuwa lugha fulani zinaonyesha kiwango cha mfanano wa namna zinavyoleksisha kijenzi cha tukio, kwa mfano jinsi usogezi unavyoelezwa katika kitenzi, haitoi sababu ya kuridhisha ya kutoa kauli za jumla kuhusu mchakato mzima katika lugha hiyo au nyingine inayoangaziwa. Kwa sababu hii ninanuia kufanya utafiti kuhusu vitendo sogezi katika Kiswahili sanifu ili kubainisha uainisho unaofaa kwa lugha hii.

## 1.3 MASWALI YA UTAFITI

a) Je, Kiswahili sanifu kinaelezaje vipengele vya vitendo sogezi vyake?

b) Je, Kiswahili sanifu huainishwa katika kundi gani kuhusiana na suala la usogezi?

c) Je, kuna uhusiano wowote kati ya mifumo ya urejelezi na njia ya usogezi?

## 1.4 MALENGO YA UTAFITI

a) Kubainisha namna ambavyo Kiswahili sanifu kinavyoeleza vipengele vya vitendo sogezi.

b) Kubainisha uainisho wa Kiswahili sanifu kwa kuhusiana na suala la usogezi.

c) Kubainisha uhusiano uliopo kati ya mifumo ya urejelezi na njia ya Usogezi.

## 1.5 UMUHIMU WA UTAFITI

Nimechagua kufanya utafiti kuhusu vitendo sogezi kwa kuwa usogezi ni mojawapo ya hali za kimsingi tunazozipitia kila siku maishani. Kutokana na hali hii nimeona ni vyema kuchunguza jinsi vitendo sogezi vinavyoelezwa katika Kiswahili.

Utafiti huu una manufaa kwa kuwa unaweka wazi uelezwaji wa vitendo sogezi katika Kiswahili sanifu. Katika utafiti huu, ninadhihirisha vipashio vinavyoleksisha vipengele mbalimbali vya vitendo sogezi katika Kiswahili sanifu. Vilevile, matokeo ya utafiti huu yanaweka msingi mwema kwa wataalamu ambao huenda watataka kufanya utafiti kuhusu namna dhana hii inavyoathiri mtazamo-ulimwengu wa watumiaji wa Kiswahili na hata utamaduni wao. Fauka ya hayo, matokeo ya utafiti huu yanadhihirisha iwapo Kiswahili ni lugha mfumbatio-tenzi au lugha mfumbatio-kifuatilizi au iwapo kinahitaji kuwekwa katika aina mpya. Kwa hivyo, unasaidia kukosoa uainishaji potovu, iwapo umetokea, wa lugha ya Kiswahili katika ule uainishaji wa Talmy.

Kwa kuwa, katika utafiti huu, ninashughulikia mada ambayo haijashughulikiwa hapo awali katika lugha ya Kiswahili, matokeo yake yanafungua milango kwa mijadala ya kiusomi na utafiti zaidi kuhusu vitendo sogezi. Kwa mfano, tafiti kuhusu jinsi watoto wanavyojifunza na kueleza vitendo sogezi katika hatua zao mbalimbali za kujifunza lugha ya Kiswahili. Vilevile, matokeo ya utafiti huu ni muhimu kwa taaluma nyingine za lugha kama vile tafsiri hasa tafsiri zinazohusu vitendo sogezi kutoka kwa lugha nyingine hadi Kiswahili sanifu. Jovanovic & Martinovic-Zic (2004) wanaeleza kuwa tofauti zilizomo kati ya lugha za mfumbatio-tenzi na zile za mfumbatio-kifuatilizi

huathiri pakubwa mtindo wa masimulizi na tafsiri kutoka au hadi kwa aina mbili hizi za lugha. Slobin (2005) anadhihirisha umuhimu wa kutafsiri masimulizi ya vitendo sogezi kwa njia inayofaa kwa kutoa mfano wa tafsiri ya sentensi inayotoa maelezo kuhusu kitendo sogezi kutoka kwa Kiingereza hadi kwa Kifaransa na kisha kurudi kwa Kiingereza na kudhihirisha jinsi inavyoonekana kupoteza maana katika tafsiri hii ya pili.

Fauka ya hayo, kuelewa namna vitendo sogezi vinavyoelezwa katika Kiswahili sanifu kunaweka wazi namna ambavyo viwango mbalimbali vya lugha hii vinavyochangia katika kueleza vitendo sogezi. Kwa hivyo, tunapata kujua ni kwa namna gani, kwa mfano, mofolojia, sintaksia na semantiki hushirikiana katika kueleza vitendo sogezi katika Kiswahili sanifu.

## 1.6 UPEO WA UTAFITI

Nilivyotaja hapo juu, utafiti huu unatuwama katika lugha ya Kiswahili sanifu. Kwa hivyo, sizingatii lahaja nyingine za Kiswahili katika utafiti huu. Mawanda ninayoyashughulikia ni ya maelezo ya vitendo sogezi na hasa namna vipengele vyake vya kisemantiki vinavyoleksishwa katika Kiswahili sanifu. Kwa hivyo, ninashughulikia maelezo ya vipengele vya vitendo sogezi, yaani umbo, chanzo, lengo, njia, namna na kisababishi kwa kutumia vipashio vya kileksia na kisintaksia. Usogezi ninaouzingatia hapa ni ule usogezi halisi bali sijumuishi usogezi dhahania au usogezi bunifu. Vilevile ninaangalia mchango wa usonde katika kueleza vitendo sogezi. Vile vile, katika huo usogezi halisi, ninajikita tu katika usogezi hamishi.

## 1.7 MSINGI WA NADHARIA

Evans & Green (2006) wanaeleza kuwa Isimu Tambuzi ni wazo la kundi la wanaisimu ambalo lilijitokeza katika miaka ya 1970 kutokana na kutoridhishwa kwa wanaisimu hao na mitazamo ya lugha iliyokuwapo wakati huo. Isimu Tambuzi imejengeka kwa mchipuko wa sayansi tambuzi na mawazo ya awali ya mwanafalsafa Gesalt pamoja na tafiti zinazohusu jinsi binadamu wanavyoainisha vitu. Isimu Tambuzi imezua nadharia mbalimbali katika uchunguzi wa lugha kama vile Nadharia ya Sarufi Tambuzi na

Nadharia ya Semantiki Tambuzi. Ninaitumia nadharia hii ya Semantiki Tambuzi katika utafiti huu.

### 1.7.1. Nadharia ya Semantiki Tambuzi

Nadharia tunayoitumia katika utafiti wetu ni ile ya Semantiki Tambuzi. Kulingana na Geeraerts (2009), Semantiki tambuzi ilijitokeza katika miaka ya 1980 kama sehemu ya Isimu Tambuzi ambayo ilipinga dai kuwa semantiki ilikuja baada ya sintaksi ilivyodaiwa katika nadharia zalishi za lugha. Talmy (2000) anaeleza kuwa nadharia hii huhusu kilichomo katika utambuzi wa binadamu na jinsi inavyopangwa katika lugha. Gardenfors (1999) anaeleza kuwa semantiki tambuzi ni tofauti na semantiki halisia. Katika semantiki halisia, maana na maelezo fulani huwa pale nje katika ulimwengu-yaani hupatikana nje ya utambuzi wa mtu. Hata hivyo, katika semantiki tambuzi maana ya maelezo huhusishwa na mifumo ya bongoni. Kiini au msingi wa Semantiki Tambuzi ni kuwa maana ya maelezo yoyote ni za bongoni. Nadharia hii huiona lugha kama sehemu ya muundo tambuzi bali si dhana inayojisimamia yenyewe.

Katika Semantiki Tambuzi, msisitizo huwekwa kwa maana za kileksia. Maana iliyo muhimu hapa ni inayohusiana na dhana iliyo ubongoni mwa mtu kulingana na uelewa wake. Baadhi ya wasomi katika uwanja wa Semantiki Tambuzi kama vile Langacker (1987) wanasisitiza kuwa mpangilio wa utambuzi wetu hutokana na tajriba zetu za kimwili. Hoja hii inamaanisha kuwa sisi binadamu huwa na mtazamo maalumu wa dunia kutokana na miundo ya miili yetu. Namna tunavyoitazama dunia huathiriwa pakubwa na miundo ya miili yetu.

Katika nadharia hii, muundo wa kisemantiki ni muundo wa kitambuzi. Kwa hivyo, maana, inavyochukuliwa hapa, imo ubongoni mwa msemaji au mtumiaji wa lugha. Muundo huu wa kisemantiki huchukuliwa kuwa kama ensaiklopidia ya aina fulani. Maneno hayawasilishi maana zinavyoonekana katika makamusi bali huwa kama mlango wa kufikia hifadhi kubwa ya maarifa kuhusiana na dhana fulani.

Allwood & Gardenfors (1999) anaeleza kuwa mfumo unaoufaa muundo wa kitambuzi ni nafasi tambuzi. Semantiki tambuzi hushadidia kuwa lugha ni sehemu ya uwezo wa kiutambuzi alio nao binadamu na huweza tu kueleza ulimwengu jinsi ilivyopangwa katika nafasi ya utambuzi. Kwa hivyo, pana tofauti kati ya ulimwengu wa kitambuzi na ule wa uhalisia. Hoja hii inatiwa nguvu na Levinson (2004) ambaye anasema kuwa fikira haiwezi kufumbatwa na lugha kwa ukamilifu.

Gardenfors (keshatajwa) anataja kuhusu vihimili vya nadharia hii.

a) Maana ni utambuzi katika Mtazamo wa Kiutambuzi. Maana si masharti ya ukweli katika dunia halisi.

Dhana kuu ya semantiki tambuzi ni kuwa: Maana zimo ubongoni. Kwa hivyo, ukweli wa kauli yoyote huchukuliwa kama jambo la pili kwa kuwa ukweli huhusu mahusiano kati ya miundo ya bongoni na ulimwengu. Kwa maneno machache, maana huja kabla ya ukweli.

b) Semantiki huja kabla ya sintaksi na huiathiri kwa kiwango fulani. Sintaksi haiwezi kuelezeka peke yake bila semantiki.

Ndani ya Semantiki Tambuzi, semantiki ndiyo kijenzi cha kwanza. Muundo wa kisemantiki huweka mipaka kwa sarufi inayoweza kutumiwa katika lugha. Kwa mfano, semantiki hudhibiti sintaksi katika jukumu la njeo.

c) Maana si huru kutoka kwa utambuzi. Msingi wa maana huwepo katika utambuzi.

Wapo wanaisimu mbalimbali ambao wametoa michango yao katika nadharia hii ya Semantiki tambuzi.

Huku akitoa mapendekezo yanayokubaliana na nadharia hii ya Semantiki Tambuzi, Talmy (1985, 1991), inayopanuliwa na kuboreshwa (2000) anapendekeza uainishaji wa lugha kwa makundi mawili kwa kuzingatia namna zinavyoeleza vitendo sogezi. Anaziainisha lugha kwa makundi mawili makuu kulingana na kipashio gani kinachoeleza dhana ya njia. Kwa hivyo, kulingana naye, lugha huweza kuwa ya mfumbatio-tenzi au mfumbatio-kifuatilizi. Tamly aliyatoa mapendekezo yake ya kwanza katika mwaka wa 1972. Anataja kuhusu hali hamishi (translatory situation).

Hali hamishi, kulingana naye ni hali ambapo umbo linasonga katika njia fulani na inaweza kuwa na vijenzi vinne vifuatavyo:

a) Umbo (U)- kitu kile ambacho kilipo kinarejelewa.

Ni kile ambacho kinachukuliwa kusonga na mahali pake, njia na mkao wake unarejelewa.

b) Msingi (M)- kitu kinachorejelewa ili kuonyesha mahali umbo lipo. Msingi ni kile ambacho umbo kinachukuliwa kusonga kwacho au kutuwama kwacho. Ni kitu cha urejelezi ambacho huwa hakisongi. Kwa mfano,

1) *Kuku yupo karibu na nyumba*.

Katika sentensi hii, *kuku* ndiye umbo huku *nyumba* ikiwa msingi.

c) Mwelekeo (Mw)- upande ambapo kitu kinachukuliwa kusonga au kuwepo kwa kuhusiana na kitu kingine.

d) Lengo (L)- mahali usogezi unaelekezwa (L)

Mfano mmoja katika sentensi unaweza kuwa:

2) *Maji yameingia ndani ya nyumba yao*.

Maji (U) yameingia (L) ndani ya (Mw) na nyumba yao (M)

Talmy (1972) anaeleza kuwa vijenzi vilivyomo ndani ya muundo wa kitendo sogezi au vilivyo nje yake vinaweza kuungana na vijenzi vya muundo huu kupitia kwa mchakato wa ufumbataji. Anaeleza kuwa ufumbataji "ni mchakato wa kisintaksi ambapo kwayo utungo changamano zaidi unabadilika na kuwa ulio sahili."

Kwa mfano,

*3) Mwanajeshi ametumbukia majini.*

Katika sentensi hii kitenzi *-tumbukia* kinafumbata maana za *kuingia majini mzimamzima bila kuacha sehemu yoyote ya mwili nje*. Kwa hivyo, kwa kutumia kitenzi -t*umbukia*, tunajiepusha na kutoa maelezo marefu na changamano. Talmy anadai kuwa katika lugha fulani kijenzi cha njia kinafumbatwa na kile cha namna katika kipashio kimoja. Kulingana na Slobin (1997), namna hurejelea mambo kama vile jinsi ya kusonga kwa umbo, kasi na kiwango cha juhudi za kusonga.

Talmy (2000) alifanya mabadiliko kidogo katika mtazamo wake huu wa awali. Anaeleza kuwa kitendo sogezi, aliloliita awali kama tukio hamishi, ni ruwaza ya vijenzi vinne, yaani umbo, usogezi, njia na msingi. Ni katika maelezo haya ambapo Talmy anatalii tofauti kati ya ufumbatio katika kitenzi na ufumbatio katika kifuatilizi. Anaeleza kuwa kuna lugha zinazofumbata usogezi na njia kama vile Kihispanyola. Vilevile, kuna vitenzi vinavyofumbata njia kwa mfano katika Kiingereza kuna vitenzi kama vile *arrive*, *enter*, *exit*, *ascend*. Njia ni usogezi hamishi ya umbo (kitu kinachosonga) kutoka kwa chanzo hadi kwa lengo. Hata hivyo, anasema kuwa vitenzi vya aina hii si vingi katika Kiingereza na huwa ya mkopo kutoka kwa Kirumi. Anatoa mifano zaidi ya lugha kama hizi kuwa ni Kisemitiki, Kipolinesia kama vile Kitamil, Kituruki, Kijapani, Kikorea na kadhalika.

Lugha za mfumbatio-tenzi ni zile zinazoeleza usogezi na njia katika kitenzi kimoja ndani ya kishazi kimoja. Katika lugha za aina hii, namna ya usogezi huelezwa kwa kipashio kingine tofauti na kitenzi katika kishazi hicho kimoja. Lugha hizi huchukua muundo ufuatao:

Kitenzi [usogezi + njia] + Kifuatilizi [namna]

Katika lugha za mfumbatio-kifuatilizi, asilimia kubwa ya vitenzi vya usogezi hueleza usogezi na namna kwa pamoja huku njia ikielezwa kwa kipashio kingine kinachofuatia katika kishazi hicho kimoja. Lugha hizi huwa na muundo ufuatao:

Kitenzi [usogezi + namna] + Kifuatilizi [njia]

Kutokana na hali hii, Genaari n.w (2001) wanaviainisha vitenzi vinavyoeleza usogezi kwa makundi mawili: vitenzi vya namna na vitenzi vya njia.

Slobin (2000) anakubaliana na uainishaji huu wa Talmy na anatoa mifano inayodhihirisha aina mbili hizi za lugha. Mifano aliyoitoa inaweza kuelezwa ifuatavyo katika Kiswahili Sanifu:

a) Lugha zilizo na muundo wa mfumbatio-kifuatilizi

| USOGEZI/NAMNA | NJIA | CHANZO/LENGO |
|---|---|---|
| ↓ | ↓ | ↓ |
| KITENZI | KIFUATILIZI | KH |
| ↓ | ↓ | ↓ |
| Wametoka | nje | ya nyumba |

b) Lugha zilizo na miundo ya mfumbatio-tenzi

| USOGEZI, NJIA | CHANZO/LENGO | NAMNA |
|---|---|---|
| ↓ | ↓ | ↓ |
| KITENZI | KH | T/E/ S |
| ↓ | ↓ | ↓ |
| Alitumbukia | kwa maji | haraka. |

Slobin (2000) anaeleza kuwa wazungumzaji wa lugha za mfumbatio-kifuatilizi wamezoeshwa na lugha zao kutofautisha namna ya kusonga, mwendo wa kusonga na tathmini kuhusu kusonga wakilinganishwa na wazungumzaji wa lugha za mfumbatio-tenzi. Hata hivyo, anasisitiza kuwa aina zote mbili za lugha zina vitenzi vinavyoeleza namna na ambavyo hutumiwa wakati ambapo namna maalumu inaangaziwa- yaani vitenzi vilivyo na maana kama *chechemea, chupa* na *chomoka*. Anaongeza kuwa lugha za mfumbatio-tenzi huwa na vitenzi vichache vinavyoeleza namna kuliko zile za mfumbatio-kifuatilizi. Hali hii, anavyoeleza, huenda imetokana na hali ya kuelezwa kwa pamoja kwa usogezi na namna katika kitenzi kwa lugha za mfumbatio-kifuatilizi imewawezesha wazungumzaji wa lugha hizo kueleza dhana hizi mbili katika nafasi hizo zilizomo katika vitenzi vya usogezi. Kufanya hivyo kunawaepushia gharama zaidi ya kueleza namna kwa kutumia vipashio vingine. Kwa upande mwingine, nafasi ya kueleza namna katika lugha za mfumbatio-tenzi ni ya hiari. Wazungumzaji wa lugha hizi hulazimika kugharamika zaidi ili kueleza namna katika sentensi zao kwa kuwa sharti waongeze kipashio au kishazi katika sentensi hizo ili kueleza namna kwa kuwa haielezwi katika vitenzi vya usogezi.

Slobin (2004) anaurutubisha uainisho huu wa Talmy na kusema kuwa kuna aina ya tatu ya lugha ambazo huweka dhana za namna na njia katika vitenzi viwili vikuu vinavyofuatana katika kishazi kimoja. Lugha hizi huitwa lugha fululiza kwa kuwa hufululiza vitenzi viwili vya usogezi katika kishazi kimoja na kugawia kila kitenzi kipengele kimoja kimoja cha njia na namna. Kwa hivyo, tofauti na aina mbili

alizozitaja Talmy, lugha fululiza hueleza njia na namna katika mizizi ya vitenzi vyao. Kimsingi ni kuwa lugha fululiza hazitumii vifuatilizi kueleza dhana za namna na njia. Kwa kiwango kikubwa, vipengele hivi huelezwa kwa kutumia vitenzi vya usogezi. Kwa sababu ya hali hii, lugha hizi, kama Kichina, hufululiza vitenzi viwili vya usogezi katika sentensi zao ili kueleza vipengele hivi viwili vya usogezi.

Slobin (2000) anaongeza kuwa lugha fululiza ni chache. Hata hivyo, wataalamu wengi hawajayakubali maoni haya ya Slobin. Kwa hivyo, wamezidi kutumia tu aina zile mbili zilizopendekezwa awali na Talmy. Kwa hali hiyo basi, lugha inaweza ikawa ya mfumbatio-tenzi au mfumbatio-kifuatilizi. Ninazingatia mawazo ya wataalamu hawa, Talmy na Slobin, katika utafiti huu.

Goschler & Stefanowitsch (2013), wakimrejelea Slobin (2000) wanaeleza kuwa lugha za mfumbatio-kifuatilizi zinapoeleza njia katika kipashio kilicho nje ya kitenzi, hutoa nafasi kwa kitenzi husika kueleza dhana zaidi kama namna. Hali hii imesababisha kuwepo kwa vitenzi vingi vinavyoeleza namna na usogezi kwa pamoja katika leksikoni ya lugha hizo. Kwa upande mwingine, lugha za mfumbatio-tenzi huwa na idadi ndogo ya vitenzi vya usogezi vinavyoeleza usogezi na namna kwa pamoja.

Vilevile, wanawanukuu Berman & Slobin (1994), wanaoongeza kuwa lugha za mfumbatio-kifuatilizi huruhusu kuelezwa kwa njia ambazo ni changamano kidogo katika KT kimoja kwa sababu njia inaelezwa kwa kutumia vipashio vilivyo nje ya kitenzi. Kwa upande mwingine, katika lugha za mfumbatio-tenzi kila njia sharti ielezwe kwa kutumia KT kingine tofauti na kile kilicho na kitenzi kilichoeleza njia ya kwanza. Hali hii inavyoaminika imesababisha kupendelewa kwa maelezo sahili ya njia katika lugha za mfumbatio-tenzi.

### 1.7.2 Mifumo ya Urejelezi

Levinson (2004) anaeleza kuwa dhana ya mifumo ya urejelezi inavyotumiwa sasa ilizuliwa na nadharia za Gesalt katika miaka ya 1920. Anasisitiza kuwa mifumo ya urejelezi inafaa maelezo ya mifumo ya pande bali si vitu vinavyorejelewa.

Anapendekeza aina tatu za mifumo ya urejelezi ambazo zinaweza kuwakilishwa kisarufi na kileksia katika lugha. Mifumo hii ya urejelezi ni muhimu katika kueleza mahusiano ya kinafasi miongoni mwa vitu vilivyomo duniani. Mifumo hiyo ya urejelezi inatokana na mitazamo mitatu tofauti. Mitazamo hii ni:

**a) Mtazamo wa kiini-mtazamaji**

Mtazamo wa kiini-mtazamaji hutumia mtazamo wa msemaji/mtazamaji kueleza mahali ambapo kitu kipo. Kwa mfano:

4) *Mtoto anacheza upande wa kushoto mwa nyumba*.

Katika mfano huu, upande wa kushoto ni upande wa kushoto wa nyumba bali si wa nyumba husika. Kwa mtazamo wa msemaji/mtazamaji, upande wa nyumba ambao mtoto anauchezea ni kushoto.

**b) Mtazamo wa kiini-kitu**

Hapa msingi unaotumiwa ni kitu kingine tofauti na mtazamaji. Kwa hivyo, zile pande zinazotumiwa kurejelea mahali kitu kipo ni zile za msingi huo husika. Kwa mfano:

5) *Ndege ametua juu ya paa la nyumba*.

**c) Mtazamo wa kiini-mazingira**

Mtazamo huu hurejelea mahali ambapo kitu kipo kwa kutumia pande zile za kimsingi, yaani kaskazini, kusini, mashariki na magharibi. Kwa mfano:

6) *Nyumba yetu inajengwa upande wa mashariki*.

Kwa kuzingatia mitazamo hii, Levinson (keshatajwa) anajitokeza na mifumo ifuatayo ya urejelezi: mfumo wa urejelezi sahili, mfumo wa urejelezi halisi na mfumo wa urejelezi husishi. Noonan (2003) anaeleza kuwa kipashio kinachobeba maana ya kipengele cha njia kinaweza kuchukua mojawapo ya mifumo hii mitatu ya urejelezi. Anaeleza kuwa mfumo wa urejelezi sahili huweza kutumiwa kurejelea kitendo cha usogezi kwa kutegemea kipengele cha msingi kwa mfano kwa *Ingia kwa nyumba* (msingi). Mfumo wa urejelezi husishi hueleza mwelekeo wa usogezi kwa kuzingatia

alipo msemaji au mtazamo wake. Mfumo huu huhusisha hasa vile vitenzi vya usonde kama vile *–ja, njoo* na *–enda*. Mfumo wa urejelezi halisi hutumia mfumo wa kueleza pande zinazohusu jiografia kama vile *–enda kaskazini, -enda mashariki* au *–enda upande wa mto.* Kwa hivyo, njia ya kitendo sogezi hapa huelezwa kwa kuzingatia msingi fulani wa kijiografia.

#### 1.7.2.1. Mfumo wa Urejelezi Sahili

Katika mfumo huu wa urejelezi, msingi na chanzo zinaelezwa pamoja. Kile ambacho ni msingi ndicho pia chanzo cha mfumo wa pande. Kwa hivyo, mfumo wa urejelezi sahili huhusisha mahusiano ya kuwili. Kwa mfano:

7) *Kamau ametoka bafuni.*

Katika sentensi hii, *bafu* ndiyo msingi na chanzo cha usogezi wa Kamau.

8) *Kuku ameingia ndani ya nyumba*.

Katika sentensi hii, *ndani ya nyumba* ndio msingi na lengo la usogezi wa *kuku*.

#### 1.7.2.2 Mfumo wa Urejelezi Halisi

Katika mfumo huu wa urejelezi, mazingira ambamo msingi hupatikana hujenga uwanja ambao umepangwa kwa namna ambayo unaweza kutumiwa kuamua uwanja wa mtazamo wa kitendo sogezi. Chanzo cha mfumo wa pande ni mazingira husika. Mifano mizuri ya mfumo wa urejelezi halisi ni kaskazini, mashariki, kusini na magharibi. Kwa mfano:

9) *Wafanyabiashara wamesafiri kuelekea kusini mwa nchi*.

#### 1.7.2.3 Mfumo wa Urejelezi Husishi

Katika mfumo huu wa urejelezi, mtazamaji ndiye chanzo cha mfumo wa pande. Pande za msemaji kama vile mbele, nyuma, kulia au kushoto zinahawilishwa hadi kwa msingi unaorejelewa. Hapa, pande za msemaji zinaweza kuakisiwa kutoka kwa msingi kana kuwa msingi wenyewe ni mtazamaji mwingine anayekabiliana na mtazamaji halisi. Kwa mfano:

*10) Mtoto wangu ananijia.*

Katika mfano huu, mwelekeo ambapo mtoto anasonga unaelezwa kwa kutumia mfumo wa urejelezi sahili. Hapa {-ni-} (mimi) ndio msingi unaotumiwa kurejelea mwelekeo wa usogezi wa mtoto. Sentensi ifuatayo pia inaweza kueleweka kwa kutumia mfumo huu wa urejelezi sahili.

Mfano mwingine tunaoweza kuutumia hapa ni:

11) *Mwizi ananitoroka*.

Hapa vilevile, {-ni-} ndio msingi na chanzo cha usogezi wa umbo. Kiambishi {-ni-} kinawakilisha "mimi" na kuonyesha kuwa mwizi anasonga kutoka kwa alipo msemaji. Kwa sababu ya usahili wa mfumo huu wa urejelezi, unapatikana katika yumkini lugha zote za ulimwengu. Nitaishughulikia dhana ya usonde katika usogezi kwa kutumia mfumo huu wa urejelezi.

Mifumo hii ya urejelezi ni muhimu katika kurejelea masuala ya usogezi ambayo ninayashughulikia katika utafiti huu. Mifano tuliyoitaja hapo juu inadhihirisha uwezekano huu.

## 1.8 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA

Wapo wanaisimu kadha ambao wamezifanyia utafiti na kuziandikia dhana ya usogezi. Kazi zao ni muhimu kwetu katika utafiti huu kwa kuwa zinatupa michango mbalimbali.

Katika sehemu hii, tunagawa mapitio yetu kwa sehemu mbili muhimu ifutavyo:

a) Maandishi yanayohusiana na vipashio vya lugha ya Kiswahili.

b) Maandishi yanayohusu dhana ya Usogezi.

### 1.8.1 Maandishi kuhusu vipashio vya Kiswahili

Massamba n.w (2001) wanashughulikia miundo ya virai na vishazi katika Kiswahili sanifu. Katika maelezo yao wanataja kuhusu KE ambacho ni muhimu kwetu katika utafiti huu. Vile vile tunafaidika na maelezo yao kuhusu vishazi vya aina mbalimbali kwa kuwa dhana tunazozitafiti zitatazamwa katika midhihiriko yao katika sentensi.

Mgullu (1999) anafanya uchambuzi wa kina kuhusu mofolojia ya maneno ya Kiswahili. Ingawa utafiti wetu hauhusu mofolojia, maelezo yake yanatufaa kwa kuwa tunapata data kuhusu vielezi, vitenzi na vihusishi ambazo ni aina za maneno yaliyo muhimu katika utafiti wetu.

Mohammed (2001), pia ametaja kuhusu vielezi na aina zao katika lugha ya Kiswahili. Maelezo yake ni muhimu kwetu katika kujenga msingi wa kazi yetu na kupata data muhimu kwa utafiti huu.

Myachina (1981) anashughulikia aina za maneno ya Kiswahili sanifu. Anaeleza kuhusu vitenzi, vielezi na vihusishi. Kwa hivyo, kazi yake pia inatupa sehemu ya data tunayoihitaji.

### 1.8.2 Maandishi yanayohusu Vitendo sogezi

Ameka & Essegbey (2013) wanachunguza dhana alizozipendekeza Talmy kuhusu uainishaji wa lugha kwa kuzingatia ni wapi zinapofumbata njia ya usogezi. Wanajumuisha pendekezo alilolitoa Slobin (2004) kuhusu kuongeza aina nyingine ya lugha kwa zile mbili alizozipendekeza Talmy. Katika utafiti wao, wanadhihirisha kuwa lugha za Akan na Ewe ni zile zinazofululiza vitenzi katika kishazi kimoja na kufumbata njia na usogezi katika vitenzi hivyo tofauti na alivyodai Talmy kuwa lugha kama hizo ni mfumbatio-tenzi.

Antunano (2009) anaeleza sababu zinazokifanya kipengele cha njia kuwa cha muhimu zaidi katika vitendo sogezi. Maelezo yake kuhusu njia yana umuhimu mkubwa kwa utafiti huu kwa kuwa njia ni kipengele kimoja kati ya vile tunavyoviangazia katika tasnifu hii.

Beavers, Levin & Tham (2009), baada ya kueleza juu ya uainishaji wa lugha alioutumia Talmy kwa kuzingatia kipengele cha usogezi cha njia, wanadadisi uwezekano wa kutumia uainishaji wa Kitalmy kuainisha lugha zote hasa kwa kuzingatia ni wapi zinapofumbata njia ya vitendo vya usogezi. Wanapendekeza kuwa swala la ni wapi lugha hufumbata njia hutegemea maswala ambayo yamo nje ya usogezi wenyewe kama vile mofosintaksi ya lugha

husika. Udadisi huu wao ni muhimu kwetu kwa kuwa unahusika na mada iliyomo katika darubini yetu.

Chen na Guo (2009) walifanya utafiti kuhusu vitendo sogezi katika riwaya za Kichina. Walipata kuwa Kichina hakingeweza kuainishwa kwa makundi mawili yaliyopendekezwa na Talmy. Walipata kuwa Kichina hufululiza vitenzi vinavyoeleza kuhusu usogezi katika kishazi kimoja. Utafiti wao ni muhimu kwetu kwa kuwa unanipa mwangaza na umakinifu zaidi tunaposhughulikia mada yetu katika Kiswahili sanifu.

Filipovic' (2007) anafanya utafiti kuhusu uleksishaji wa vitendo sogezi katika lugha mbalimbali. Anataja kuhusu njia mbalimbali za uleksishaji wa vipashio vya usogezi, yaani namna na njia. Vile vile, anatoa maelezo kuhusu fasili za dhana ya vitendo sogezi. Kwa kuwa tunaviangazia dhana hizi katika utafiti huu, maelezo anayoyatoa ni ya natija kwetu.

Fortis (2010) anatalii uanishaji wa lugha uliofanywa na Talmy (keshatajwa) na kuonyesha maendeleo yake. Anajumuisha mapendekezo aliyoyatoa Slobin (2004) kuhusu namna ya kuboresha uainishaji huo wa Talmy ili kuhusisha lugha ambazo zinaleksisha namna na njia katika mfululizo wa vitenzi. Vilevile, anadhihirisha baadhi ya hali anazoziona kuwa pungufu katika uanishaji wa Talmy. Anaorodhesha matatizo saba anayoyaona katika uainishaji wa Talmy. Kazi yake ni muhimu kwetu kwa kuwa anatoa maelezo kuhusu nadharia tunayoitumia katika utafiti huu na hivyo kutusaidia kuielewa zaidi.

Goschler & Stefanowitsch (2013) wanatoa maelezo kuhusu athari za uleksishaji wa usogezi katika lugha ya kwanza ya mtu (L1) na inavyoathiri jinsi mtu husika anavyoeleza dhana ya usogezi katika lugha yake ya pili (L2). Hata hivyo, wanatoa maelezo ya kina kuhusu lugha za mfumbatio-tenzi na mfumbatio-kifuatilizi. Maelezo haya ni muhimu kwa utafiti wetu. Wanaeleza zaidi kuhusu uainishaji wa Talmy kwa kutumia kipashio kinachoeleza njia ya kitendo sogezi. Wanakubaliana na Talmy kuwa lugha za dunia hugawika kwa aina mbili. Kuna lugha ambazo wazungumzaji wake hutumia vitenzi ambavyo mizizi yake hueleza njia inayochukuliwa na kile kinachosonga. Wanasema kuwa maelezo zaidi kuhusu kitendo sogezi

husika yanatolewa na kipashio kingine tofauti na kitenzi kikuu. Wanaongeza kuwa kuna lugha zile ambazo wazungumzaji wake hueleza njia katika kipashio kilicho nje ya mzizi wa kitenzi. Kwa hivyo, katika lugha kama hizi, kitenzi cha usogezi kinaeleza tu kuwa kitendo sogezi limetokea na kinaweza kuongeza namna ya kutokea kwa kitendo sogezi husika.

Hoffmann (2011) anaeleza kuhusu maelezo ya usogezi na usafiri katika Jaminjung na Kriol. Katika kazi yake anafanya utafiti wa kina kuhusu usogezi na kudhihirisha jinsi ambavyo usonde na mifumo ya urejelezi zinavyojitokeza katika uelezaji wa usogezi katika lugha hizi mbili. Maelezo anayoyatoa ni muhimu kwangu hasa katika kuangalia namna usonde na mifumo ya urejelezi inavyohusika katika kueleza usogezi katika Kiswahili sanifu.

Jackendoff (1983) anaeleza kuhusu nadharia ya Semantiki Tambuzi ambayo tunaitumia katika utafiti huu. Maelezo yake ni muhimu kwetu kwa kuwa yanatupatia uelewa mpana wa nadharia hii.

Mateu & Matellan (2012) wanashughulikia namna inavyoelezwa katika lugha. Wanaeleza kuwa kuelezwa kwa namna katika kitenzi hutegemea pakubwa kanuni za kisintaksi zilizomo katika lugha. Wanaorodhesha na kufafanua baadhi ya kanuni hizo za kisintaksi. Maelezo yao ni muhimu kwetu katika utafiti huu kwa kuwa yanatusaidia kupata maelezo ya kina kuhusu dhana ya namna na vile inavyoweza kuelezeka katika lugha na kutuwezesha kutoa sababu za hali hii.

Ngina (2015) alifanya tathmini ya kisemantiki ya maelezo ya nafasi katika lugha ya Kikamba. Ijapokuwa alishughulikia nafasi katika utafiti wake, kazi yake bado ni muhimu kwetu kwa kuwa dhana za usogezi na nafasi huhusiana kwa namna fulani. Fauka ya hayo, utafiti wake ameufanya kuhusu Kikamba ambacho ni mojawapo ya lugha za Kibantu sawa na Kiswahili na ametoa maelezo kuhusu mifumo ya urejelezi.

Noonan (2003) amefanya utafiti kuhusu vitendo sogezi katika lugha ya Chantyal inayozungumzwa nchini Nepal. Anaeleza kuwa suala la usonde katika usogezi linaweza

kushughulikiwa katika mifumo ya urejelezi. Anatoa mifano ambayo inatupa mwelekeo muhimu kuhusu usonde na usogezi ambazo ni dhana muhimu katika utafiti huu.

Papafragou n.w (2002) wanachunguza iwapo hali ya lugha kuwa ya mfumbatio tenzi au mfumbatio kifuatilizi huathiri namna ambavyo wazungumzaji wa lugha hizo huelewa usogezi. Wanalinganisha jinsi watoto na watu wa umri wa makamu wanaozungumza Kiingereza na wanaozungumza Kigiriki wanavyoeleza usogezi kwanza kwa kutumia njia zisizo za lugha na pili kwa kutumia lugha. Wanapata kuwa ingawa wazungumzaji wa lugha hizi mbili walieleza vitendo sogezi kwa namna tofauti sana kwa kutumia lugha zao, maelezo yao kuhusu vitendo sogezi kwa kutumia njia zisizo za lugha yalifanana. Kwa hivyo, utafiti wao ni muhimu kwa utafiti huu kwa kuwa, kutokana nao, tunaelewa kuwa kila lugha huweza kueleza Vitendo sogezi kwa vipashio vilivyomo ndani yake tofauti na lugha nyingine. Huenda basi tofauti kati ya lugha moja na nyingine kuhusu namna ya kueleza usogezi unatokana na tofauti zilizomo ndani ya lugha hizo bali si utambuzi wa wazungumzaji wa lugha husika.

Papafragou n.w (2006) wanashughulikia dhana za usogezi na maelezo ya njia na Namna katika vitenzi vya Kiingereza na Kigiriki. Wanaeleza na kutoa mifano ya namna lugha mbalimbali zinavyoleksisha dhana ya njia. Wanaeleza kuwa lugha za mfumbatio-tenzi huwa na vitenzi vingi vinavyoeleza usogezi na njia kwa pamoja huku zikiwa na vitenzi vichache vinavyoeleza usogezi na namna kwa pamoja. Lugha za mfumbatio-kifuatilizi, kulingana nao, huwa na vitenzi vingi vinavyoeleza usogezi na namna pamoja huku zikiwa na vitenzi vichache vinavyoeleza usogezi na njia kwa pamoja. Utafiti wao ni muhimu kwangu kwa kuwa dhana wanazozishughulikia zinahusiana na mada ninayoifanyia utafiti.

Slobin (2000) anatoa ufafanuzi wa kina kuhusu uleksisishwaji wa usogezi katika lugha. Anaeleza kuwa maelezo ya namna katika lugha hutegemea pakubwa ruwaza ya uleksisishaji katika lugha husika. Anaeleza kuwa ruwaza hizi huathiri namna watu wanavyofikiri ili kuongea. Anaeleza vilevile kuwa ruwaza hizi huwafanya wazungumzaji wa lugha kushughulikia matukio ya usogezi zinazoelezwa katika lugha. Msimamo wake ni kuwa katika lugha za mfumbatio-tenzi, nafasi ya kitenzi huchukuliwa na kitenzi kinachoeleza Njia katika mzizi wake. Kitenzi kinachoeleza namna katika mzizi wake hutumiwa tu kama kitenzi kikuu

ikiwa tu kishazi husika hakielezi badiliko la mahali pa umbo. Maelezo haya ya Slobin ni muhimu kwa utafiti huu hasa katika kushughulikia vitenzi vya usogezi.

Slobin (2005) anashughulikia dhana za kiashiria na kiashiriwa katika maelezo ya vitendo sogezi. Maelezo yake yananipa mwelekeo na uelewa zaidi kuhusu mada yetu kwa kuwa anashughulikia vipengele ninavyoviangazia.

Talmy (1991) anaeleza kwa tafsili dhana ya uelezaji wa njia katika lugha. Maelezo anayoyatoa ni muhimu kwetu kwa kuwa uelewa mwema na wa kina wa dhana hii unatoa mchango mkubwa katika kufanikisha utafiti huu.

Talmy (2000), anatoa jumuisho la kazi zake alizoziandika katika uwanja wa semantiki kwa takribani miaka ishirini. Anarejelea jinsi lugha zinavyoeleza usogezi. Anazingatia hasa vihusishi vinavyohusiana na usogezi. Vilevile, anataja kwa kina kuhusu dhana za umbo na msingi katika lugha. Maelezo yake ni muhimu kwetu kwani yanaangazia masuala yanayohusiana na ninayoyashughulikia katika utafiti huu.

Zlatev na Yangklang (2004) wanaorodhesha baadhi ya tofauti zinazojitokeza kati ya lugha zinazoleksisha njia katika vitenzi na zile zinazoleksisha njia katika vifuatilizi. Mchango wao ni muhimu huu hasa kwa kuwa ninalenga kutathmini ukweli wa madai yaliyotolewa awali na wanaisimu kuhusu lugha ya Kiswahili kuwa mfumbatio-tenzi.

## 1.9 NJIA ZA UTAFITI

Nitatumia njia tatu za kukusanya data zilizo muhimu kwa utafiti huu.

### 1.9.1 Jaribio la Kwanza

Katika jaribio hili niliwahusisha wanafunzi kumi wa Shule ya Upili ya Brucewood na wengine watano wa Chuo Kikuu cha Nairobi ili kupata sentensi ambamo vitenzi husika vya usogezi vimetumika. Washiriki walipewa orodha ya vitenzi vya usogezi vya Kiswahili sanifu thelathini na vitatu (33) na kuombwa kuzitungia sentensi mbalimbali,

yaani sentensi tatu tatu kwa kila kitenzi cha usogezi. Nilivichagua vitenzi hivi kwa kuwa ndivyo hutumika mara nyingi katika Kiswahili sanifu. Kwa hivyo, hivi si vitenzi vyote vya usogezi katika Kiswahili sanifu. Kutokana na sentensi za washiriki, nilichagua zile za kuchanganua kwa kuangalia maelezo ya vipengele vya vitendo sogezi ndani yao. Jaribio hili lilinipa uwezo wa kukusanya data muhimu kuhusu matumizi ya vitenzi vingi vya usogezi kwa muda mfupi ambao ni muhimu kwa utafiti huu. Baadhi ya sentensi walizozitunga zilieleza vitendo sogezi mbalimbali kwa kutumia vitenzi nilivyowapa. Vilevile, idadi hii ya washiriki ilinipa sentensi nyingi za Kiswahili zinazoeleza vitendo sogezi.

**1.9.2 Jaribio la Pili**

Pili, nilikusanya data kwa kutumia hadithi ya picha ya *Frog, Where Are You?* (*Upo wapi chura?*) iliyoandikwa na Mayer (1969). Kitabu hiki kimetumiwa na watafiti wengine wengi kama vile Berman na Slobin (1994) kufanya utafiti kuhusu vitendo sogezi katika lugha mbalimbali.Watafiti hao waliwapa washiriki wa tafiti zao kitabu hiki na kuwaomba wakasimulie matukio yaliyomo katika picha za kila ukurasa huku wakirekodi sauti zao. Kwa namna hii waliweza kutoa maelezo mbalimbali ya vitendo sogezi vilivyomo katika picha za kitabu hicho.

Matukio yaliyomo katika *Frog, Where Are You?* yanatoa nafasi nyingi za kutoa maelezo ya Vitendo sogezi. Katika hadithi hii ya picha, chura anayefugwa na mvulana anatoroka kutoka katika chupa yake. Mvulana anapogundua kuwa chura hayupo, yeye pamoja na mbwa wake wanaanza kumtafuta. Katika mchakato huu wa kumtafuta chura, mvulana na mbwa wanapitia matukio kama vile kuanguka kutoka dirishani, kupanda na kuanguka kutoka mtini, kutumbukia majini, kufukuzwa na nyuki na kuvuka mto.

Katika Jaribio hili, niliwapa washiriki nakala za kitabu hiki na kuwaomba kusimulia yanayotendeka katika picha za kurasa zote 29 ambazo zina picha mbalimbali zinazoonyesha vitendo sogezi. Niliwahusisha wanafunzi watano wa Chuo Kikuu cha Nairobi. Kila mmoja wao aliandika maelezo yake kwa kuzingatia mfuatano wa kurasa za kitabu hiki. Kutokana na maelezo yao ya visa vinavyotendeka katika kila ukurasa, nilidondoa sentensi zinazorejelea vitendo sogezi na kuangalia jinsi vipengele vyake vilivyoelezwa katika kila sentensi. Jaribio hili liliniwezesha kupata data katika

muktadha wa masimulizi japo katika maandishi. Data za aina hii zilikuwa muhimu kwa utafiti huu kwa kuwa zilitoa maelezo mapana kuhusu vitendo sogezi na huweza kudhihirisha vipengele vyote vya usogezi ambavyo nilivishughulikia humu.

Hata hivyo, ili kufidia mapungufu yoyote yanayoweza kukumba Jaribio la Kwanza na Jaribio la Pili, sehemu ndogo ya data muhimu niliijenga mwenyewe kutokana na ujuzi wangu kama mtaalamu wa lugha ya Kiswahili sanifu. Nilitafuta ushauri wa wataalamu wa lugha ili kuhakikisha kuwa data zote nilizozitumia ni sahihi na kuwa ilichaguliwa bila mapendeleo yoyote.

Nilizichanganua sentensi nilizozipata kwa njia hizi tatu kwa kutumia vipengele vilivyomo ndani ya nadharia ya Semantiki Tambuzi vilivyoelezwa na Talmy katika uainishaji wake wa lugha kwa kuzingatia maelezo ya Vitendo sogezi.

## SURA YA PILI

## 2.0 VIPENGELE VYA VITENDO SOGEZI

### 2.1 Utangulizi

Katika sura ya kwanza nimefanya utangulizi wa dhana ya kitendo sogezi na vipengele vyake kwa jumla na kutaja tatizo la utafiti huu. Vile vile, nimetaja kuhusu baadhi ya maandishi na tafiti za wataalamu mbalimbali kuhusu vitendo sogezi. Kwa hivyo, katika sura hii ya pili, ninaangalia vipengele hivyo vya vitendo sogezi katika Kiswahili sanifu kimoja baada ya kingine. Je, ni vipashio vipi vinatumiwa kuvieleza vipengele vya vitendo sogezi katika lugha ya Kiswahili? Vilevile, nitatoa ufafanuzi wa kina wa aina na matumizi ya vitenzi mbalimbali vya usogezi katika Kiswahili.

### 2.2 Maelezo

Talmy (1985, 2000) anaeleza kuwa maelezo ya vitendo sogezi huhusisha vipengele vinne: i) umbo (ii) usogezi (iii) njia ya usogezi na (iv) msingi. Msingi huwa na sehemu mbili- chanzo na lengo. Kimsingi, njia huwa kati ya chanzo na lengo. Ni njia ndiyo huunganisha chanzo na lengo katika kitendo sogezi. Hivi vipengele vinne ambavyo nimevitaja hapo juu vimeorodheshwa na Talmy kama vipengele vya ndani vya kitendo sogezi. Hata hivyo, anaviongeza vipengele vingine viwili ambavyo anavieleza kuwa ni vya hiari katika kitendo sogezi. Vipengele hivyo ni namna na kisababishi cha usogezi. Vipengele hivi ni vya nje katika kitendo sogezi. Ni vipengele ambavyo huelezwa tu palipo na haja kubwa ya kuvieleza, hasa palipo na umuhimu wa kutoa maelezo mahususi. Kwa hivyo, tunaweza kusema kuwa vipengele vinne vya kwanza ni vya hadhi ya juu zaidi ya hivi viwili vya mwisho.

Talmy (keshatajwa) anaeleza kuwa hivi vipengele vya kitendo sogezi ni vipengele vya kisemantiki vilivyomo katika utambuzi wa wazungumzaji wa lugha. Anaongeza kuwa hivi vipengele sharti vielezwe kwa kutumia vipengele vingine vilivyo dhahiri (vya kileksia na kisintaksia) katika lugha husika. Vipengele vya kileksia na kisintaksia ambavyo hubeba vile vya kisemantiki ni kama vile vitenzi, vifuatilizi, virai, viambishi na vishazi vitegemezi. Kwa hivyo, ni vyema kuangalia ni vipengele vipi vya kileksia na kisintaksia vinavyotumiwa kubeba vile vya kisemantiki katika lugha ya Kiswahili. Anavyoeleza Talmy (keshatajwa), kipengele

kimoja cha kisemantiki huweza kubewa na kipengele kimoja au zaidi vya kileksia au kisintaksia. Vilevile, vipengele viwili au zaidi vya kisemantiki huweza kubebwa na kipengele kimoja cha kisintaksia. Kwa mfano:

12) *Matawi yanaelea majini kuelekea magharibi*.

*Matawi* [umbo] *yanaelea* [usogezi + namna] *majini* [msingi] *kuelekea* [njia] *magharibi* [lengo].

13) *Baba na mama wanarudi walikotoka*.

*Baba na mama* [umbo] *wanarudi* [usogezi + njia] *walikotoka jana* [lengo].

Kulingana na Talmy, vipengele vya umbo, njia, usogezi na msingi hupatikana katika kila kitendo sogezi. Hata hivyo, kauli hii ya Talmy haimaanishi kuwa vipengele hivi sharti vijitokeze kwa vipashio vya lugha kila wakati wa kueleza kuhusu kitendo sogezi. Anasema kuwa vinaweza kuelezwa waziwazi au vikafichwa kwa namna ambavyo havidhihiriki waziwazi kwa kutumia vipashio vya lugha katika kueleza kitendo sogezi husika. Kwa mfano, tunaweza kuwa na sentensi kama ifuatayo inayoeleza kuhusu kitendo sogezi.

*14) Mama ametembea kutoka mtoni hadi nyumbani.*

*Mama* [umbo] *ametembea* [usogezi+namna] + *kutoka* [njia] *mtoni* [chanzo] *hadi* [njia] *nyumbani* [lengo].

Hata hivyo, katika miktadha mbalimbali na kwa sababu mbalimbali za kisemantiki, tunaweza kuficha vipengele vingine vya kitendo sogezi hiki. Kwa mfano:

*15)Mama ametembea hadi nyumbani*.

*Mama* [umbo] *anatembea* [usogezi+namna] *hadi* [njia] *nyumbani* [lengo].

Kwa hivyo, katika sentensi hii, kipengele cha chanzo kinakosa kujitokeza waziwazi kisintaksia, yaani hatujaleksisisha kipengele cha chanzo. Hata hivyo, kipengele hiki kipo katika muundo wa ndani wa kisemantiki wa kitendo sogezi hiki na wasikilizaji wanaweza kukipata kwa kurejelea muktadha wa mazungumzo. Mfano mwingine ni sentensi ifuatayo:

*16) Auma, Katito haraka!*

Kitenzi cha usogezi katika sentensi hii kimedondoshwa lakini msikilizaji wa sentensi hii, kwa kuzingatia muktadha, ataelewa muundo wa ndani (wa kisemantiki) wa sentensi hii na kufahamu kuwa kitenzi husika hapa ni *enda* au *kimbia*. Tunaweza kueleza kuwa vipengele vya Vitendo sogezi vinajitokeza kwa namna ifuatayo katika sentensi hii:

*Auma* [umbo] Ө [kitenzi cha usogezi] *Katito* [lengo] *haraka* [namna].

**2.2.1 Usogezi**

Lenz (2003:x) anaeleza kuwa usogezi unaweza kuelezwa kama badiliko la mahali ambapo kitu kipo kwa mpito wa wakati. Anaongeza kuwa kueleweka kwa usogezi huhitaji mfululizo changamano wa matukio ya kiwakati na kinafasi. Usogezi unaweza kuwa kwa mielekeo mbalimbali. Usogezi unaweza kutendeka katika Njia mlalo. Kwa mfano:

17) *Wanja anaenda mtoni*.

*Wanja* [umbo] *anaenda* [usogezi + njia] *mtoni* [lengo].

Vilevile, usogezi huweza kutokea kwa mwelekeo wa kuingia ndani ya kitu. Kwa mfano:

18) *Kiboko ametumbukia majini*.

*Kiboko* [umbo] *ametumbukia* [usogezi + njia] *majini* [lengo].

Mwelekeo wa tatu unaoweza kuchukuliwa na Usogezi ni wa chini-juu/juu-chini.

19) *Nyani anaukwea mwembe*.

*Nyani* [umbo] *anaukwea* [usogezi + njia] *mwembe* [lengo].

20) *Mgema anashuka kutoka juu ya mnazi*.

*Mgema* [umbo] *anashuka* [usogezi + njia] *kutoka* [njia] *juu ya mnazi* [chanzo].

Usogezi vilevile unaweza kuchukua muda fulani kutendeka wakati ambapo Umbo linasonga kutoka sehemu moja hadi nyingine au ukawa Usogezi wa kufululiza. Kwa mfano:

21) *Ndege ilipaa angani kwa dakika chache*. (unatendeka kwa muda kisha unakoma)

*Ndege* [umbo] *ilipaa* [usogezi + namna] *angani* [lengo] *kwa dakika chache*.

22) *Mwanafunzi anaendelea kutembea*. (usogezi unaendelea)

*Mwanafunzi* [umbo] *anaendelea* [usogezi + njia] *kutembea* [usogezi + namna].

Talmy (2000), anagawa usogezi kwa aina mbili. Anasema kuwa usogezi unaweza kuwa hamishi au tuwami. Usogezi hamishi hutokea wakati ambapo kitu (umbo) kinatoka mahali pa awali hadi mahali pengine kwa muda fulani. Usogezi huu huhusisha badiliko la nafasi inayochukuliwa na umbo na kwamba badiliko hilo linahitaji muda fulani ili kutendeka. Sentensi ya *Ndege ilipaa angani kwa muda mchache* ni mfano mzuri hapa.

Usogezi tuwami hutokea wakati ambapo kitu (umbo) kinadumisha nafasi yake ya kimsingi awali. Usogezi huu huhusisha mifano kama *kutingisika, kuyumbayumba*, *kutetemeka, kupanuka* na *kubanika* na kadhalika. Kitu kinaweza kutetemeka au kutingisika lakini likasalia palepale kilipokuwa. Kwa mfano:

23) *Taa ilitingisika darini ilipogongwa*.

Usogezi hamishi na tuwami huweza kutokea kwa wakati mmoja katika kitendo sogezi kimoja. Kwa mfano:

24) *Mwanafunzi <u>alikimbia</u> <u>akitetemeka</u> alipoitwa na mwalimu*.

Kitenzi *kimbia* kinarejelea usogezi hamishi huku kitenzi *tetemeka* kikirejelea usogezi tuwami. Hata hivyo, katika utafiti huu, aina ya usogezi ulio muhimu kwangu ni usogezi hamishi.

### 2.2.2 Umbo

Umbo hurejelea kile kitu kinachosonga katika kitendo sogezi. Kwa mfano:

25) *<u>Farasi</u> ameruka ua.*

*Farasi* [umbo] *ameruka* [usogezi + namna] *ua* [msingi-pitwa].

26) *Mwanariadha amerusha <u>tufe</u>.*

*Mwanariadha* [kisababishi] *amerusha* [usogezi + namna] *tufe* [umbo].

Ungerer & Schimid (1996:20) wanaeleza kuwa umbo ni kipengele cha lazima katika kila kitendo sogezi. Wanasisitiza kuwa hapawezi kuwa na usogezi bila kuwapo kwa umbo. Hata hivyo, wanaongeza kuwa umbo linaweza kuwapo bila kuwa na usogezi wowote. Maelezo haya ya Ungerer na Schimid yanamaanisha kuwa tunaweza kufasili upya istilahi hii ya umbo la kitendo sogezi. Fasili tuliyoitoa awali ilieleza kuwa umbo ni kitu kile kinachosonga na mahali pake, njia na mkao wake unarejelewa. Kwa hivyo, kulingana na fasili hiyo, umbo ni istilahi iliyo na maana tu wakati kunapotokea kitendo sogezi. Iwapo hapana kitendo sogezi basi hapana umbo vilevile. Hivyo basi, kitu huwa umbo tu wakati kinaposonga bali si umbo wakati kimetuwama mahali. Tunaweza kusema, hivyo basi, kuwa umbo na usogezi ni mambo mawili yasiyotenganishika.

Hata hivyo, mawazo ya Ungerer na Schimid (keshatajwa) yanatupa mawanda mapana ya kuifasili dhana ya umbo. Swali moja ambalo laweza kufaa hapa ni kuwa, Je, kitu huwa umbo tu wakati kinaposhiriki katika kitendo sogezi au huwa umbo hata kabla ya kushiriki katika kitendo sogezi? Ili kujibu swali hili, ni vyema tukaangalie sifa ambazo sharti kitu fulani kiwe nazo ili kiweze kuwa umbo katika kitendo sogezi. Kimsingi, hizi ndizo sifa za umbo katika kitendo sogezi.

Kwanza kabisa, umbo lazima liwe na uwezo wa kusonga (kama vile binadamu au wanyama) au uwezo wa kusongezeka. Pili, umbo halitenganishiki kutoka kwa kitendo sogezi, yaani ukilitoa umbo katika kitendo sogezi basi hapatakuwa na kitendo sogezi. Sifa ya tatu ni kuwa umbo linaweza kuwa katika hali ya kutuwama (linaweza kushiriki katika usogezi bila kuondoka mahali pake pa awali) au likatoka sehemu moja hadi nyingine katika usogezi. Wakati ambapo umbo limetuwama mahali bila kuhama bado ni umbo ila tu kwamba halisonga kutoka sehemu moja hadi nyingine kama katika mfano wa hapo juu, *Taa ilitingisika darini ilipogongwa*. Hapa *taa* ndiyo umbo lakini haijatoka kwa dari hadi sehemu nyingine. Hata hivyo, katika kutuwama huko, kina uwezo wa kusonga au kusongezeka kutokana na kisababababishi.

Kutokana na maelezo haya, ninaifasili umbo, katika tasnifu hii, kama kitu kilicho na uwezo wa kusonga na kinasonga au kitasonga au kilisonga kutoka sehemu moja hadi nyingine au kisonge pale tu kilipo au kitasogezwa katika kitendo sogezi. Sentensi kama

ifuatayo ambayo inaeleza kitendo sogezi bado itakuwa sahihi hata kama kwa wakati wa kuongea umbo litakuwa limetuwama mahali fulani.

27) *<u>Nyani</u> atashuka kutoka mtini*.

*Nyani* [umbo] *atashuka* [usogezi + njia] *kutoka* [njia] *mtini* [chanzo].

Sentensi hii inaonyesha kuwa *nyani* hajaanza kusonga wakati wa kusemwa kwa sentensi hii lakini atafanya hivyo muda fulani baada ya kusemwa kwake. Hata hivyo, *nyani* bado ni umbo katika kitendo sogezi hiki.

Katika lugha ya Kiswahili, kipengele cha umbo kinaweza kuainishwa katika makundi mawili makuu kwa kutumia kigezo cha kisemantiki. Makundi hayo ni:

a) Wanyama na binadamu

b) Viumbe visivyo-hai, miti na mimea

Katika kundi la kwanza, umbo linalopatikana huwa na uwezo wa kujisogeza lenyewe bila msaada wa kitu kingine. Mifano ifuatayo ya sentensi inaonyesha hali hii. Umbo linaonyeshwa kwa kupigia kistari neno husika.

28) *<u>Punda</u> anakimbia uwanjani*.

29) *<u>Mdudu</u> anatambaa nguoni*.

Katika sentensi hizi mbili, kitu ambacho ni umbo lina uwezo wa kushiriki katika kitendo sogezi kwa hiari yake. Hata hivyo, umbo la aina hii pia huweza kupatikana katika vitendo sogezi vinavyohusu usogezi wa kusababishwa. Jerono (2017) anaeleza kuwa kitendo sogezi sababishwa hurejelea badiliko la mahali ambapo kitu kipo kutokana na athari za kitu kingine. Ninatoa mifano ya sentensi kudhihirisha hali hii.

30) *Baba anamwangusha <u>punda</u> shambani*.

31) *Buibui anamvuta <u>mdudu</u> ukutani*.

Katika sentensi zetu za hapo juu, *punda* na *mdudu* wanasonga kwa sababu kuna kitu kingine ambacho kimewachochea kusonga.

Kundi la pili la umbo huhusisha mimea na vitu visivyokuwa hai kama vile mawe, upepo, maji na miti. Hivi ni viumbe visivyoweza kushiriki katika vitendo sogezi vya hiari. Ili viweze kusonga, sharti kuwepo na kisababishi kitakachovichochea kusonga

kutoka sehemu moja hadi nyingine. Hata *mto* ambao huonekana kutiririka tu hauwezi kutirika bila kuwapo kwa kani za mvuto au mteremko fulani. Kwa hivyo, kusonga kwa *mto* au kutiririka kwa *maji* yake kunategemea nguvu nyingine isiyoamuliwa na *mto* au *maji*. Mifano ifuatayo ya sentensi ni muhimu katika kueleza aina hii ya umbo.

32) *Upepo umepeperusha karatasi kutoka kitini*.

33) *Mchezaji aliurusha mpira*.

### 2.2.3 Chanzo

Hoffman (2011:19) anaeleza chanzo kama, "Sehemu inayochukuliwa kuwa mwanzo wa kitendo sogezi kama vile *kutoka kwa nyumba*." Kwa hivyo, chanzo ni mahali ambapo kitendo cha usogezi kinachorejelewa kinapoanzia. Kimsingi, chanzo ni mwanzo wa njia ya usogezi. Tafiti za awali zimedhihirisha kuwa kipengele cha chanzo cha kitendo sogezi huwa kinapuuzwa sana katika maelezo na masimulizi yanayohusu vitendo sogezi kuliko kile cha lengo. Tafiti kama hizo zimefanywa na wataalamu kama vile Lakusta n.w (2007) ambao wanaeleza kuwa watoto aliowatumia katika utafiti wake walionyesha mapendeleo kwa lengo katika sentensi zilizohitaji maelezo ya chanzo na lengo kwa pamoja. Papafraguo (2010) naye alifanya utafiti unaokaribiana na huo wa Lakusta ila kwamba aliwatumia watoto walio na ugonjwa wa William Syndrome na watoto wasiokuwa na ugonjwa huo. Matokeo yake yalikuwa sawa na ya Lakusta n.w (keshatajwa). Wazungumzaji wa lugha zilizofanyiwa utafiti walidhihirisha chanzo katika sentensi mara chache kuliko jinsi walivyoeleza lengo. Hata hivyo, matokeo hayo hayamaanishi kuwa chanzo hakina maana katika maelezo ya vitendo sogezi. Chanzo bado huleksishwa wazi katika sentensi za lugha, kama Kiswahili sanifu, wakati wa kueleza kuhusu vitendo sogezi. Swala la kueleza chanzo au kutoeleza ni la chaguo na hutegemea muktadha wa mazungumzo au kile ambacho mzungumzaji wa lugha husika anataka kukipa uzito. Vipo vitenzi vya usogezi vya Kiswahili ambavyo kwa namna moja au nyingine sharti viandamane na neno au kirai kinachorejelea chanzo cha kitendo sogezi husika huku kukiwa na vingine vinavyokihitaji kwa hiari tu.

Kuna vipashio mbalimbali vinavyohusika katika kuleksisha chanzo cha vitendo sogezi katika Kiswahili sanifu. Kimsingi, chanzo cha vitendo sogezi huelezwa kwa kutumia KH, KE na kishazi kitegemezi.

#### 2.2.3.1 Maelezo ya Chanzo kwa KH

Vipo vihusishi ambavyo huhusika katika kueleza Chanzo cha Kitendo sogezi. Vihusishi hivyo hushirikiana na nomino au KN ili kueleza Chanzo. Vihusishi vinavyohusika hapa ni kama vile *kutoka* na *kuanzia*. Kwa mfano:

34) *Kamau alisafiri <u>kutoka Nairobi</u> hadi Kisumu*. (KH)

*35) Wanyama wanahama <u>kutoka mbuga moja</u> mpaka nyingine. (KH)*

#### 2.2.3.2 Maelezo ya Chanzo kwa Kielezi au KE

Chanzo cha usogezi pia huweza kuelezwa kwa kutumia kielezi au KE. KE husika kinaweza kuwa cha maneno mawili au zaidi. Kwa mfano:

36) *Baba ametoka <u>Nairobi</u> leo asubuhi*. (Nairobi- Kielezi cha mahali)

37) *Vyura wametoka <u>mafichoni mwao</u>.* (KE)

Kielezi hapa ni *Nairobi* huku KE kikiwa *mafichoni mwao*.

#### 2.2.3.3 Maelezo ya Chanzo kwa Kishazi kitegemezi

Lugha Kiswahili pia hutumia vishazi vitegemezi vinavyoeleza kuhusu mahali ili kueleza chanzo cha kitendo sogezi. Kwa mfano:

38) *Mvulana alitoka <u>alipokuwa mbwa</u>*.

39) *Alitembea kuanzia <u>alipokuwa akisimama</u>*.

Katika sentensi hizi mbili, chanzo kinaelezwa kwa kutumia vishazi vitegemezi *alipokuwa mbwa* na *alipokuwa akisimama*.

### 2.2.4 Lengo

Hoffman (201:19) analifasili lengo kuwa ni "...msingi ambapo kitendo sogezi kinaelekezwa na ambacho kinaweza kufikiwa au kutofikiwa." Nam (2004:02) anaeleza kuwa, "Ikiwa tukio linahusisha kusonga kwa kitu na njia ya kusonga huko, lengo hurejelea sehemu ya mwisho ya Njia hiyo...." Kwa hivyo, kulingana naye, lengo ni sehemu ile ambayo usogezi unamalizikia. Stefanowitsch & Rhode (2004) wanaeleza kuwa kumekuwapo na madai kuwa kipengele cha vitendo sogezi cha lengo

hupendelewa katika maelezo yanayotolewa kuhusu usogezi katika lugha. Utafiti katika lugha mbalimbali umeonyesha, kwa mfano, kuwa KH vinavyoeleza lengo hutumiwa zaidi kuliko vile vinavyoeleza chanzo cha usogezi. Tumetaja mifano ya tafiti mbili hapo juu zilizofanywa na Lakusta n.w (keshatajwa) na Papafraguo (keshatajwa) kuhusu vipengele hivi vya chanzo na lengo. Stefanowitsch & Rhodes (keshatajwa) wanawarejelea Verspoor, Dirven & Radden (1999:88) ambao wanatoa mifano mitatu ya sentensi kuonyesha hali hii ya kupendelea kutoa maelezo kuhusu lengo kuliko maelezo ya vipengele vingine vya vitendo sogezi.

40) a) *Nilipanda <u>kutoka</u> chumbani mwangu kwa ngazi <u>hadi</u> paani*. (TY)

b) *Nilipanda <u>hadi</u> paani*. (TY)

c) *Nilipanda <u>kutoka</u> chumbani mwangu*. (TY)

Wanafafanua kuwa sentensi ya (1a) inaeleza kwa uwazi vipengele vyote vinne vya Vitendo sogezi, yaani njia, chanzo (kutoka chumbani), mwelekeo na lengo (paa). Sentensi ya (1b) na (1c) zinaonyesha kuwa inawezekana kueleza njia au lengo tu lakini haiyumkiniki au haikubaliki kisemantiki kueleza chanzo pekee yake. Verspoor, Dirven & Radden wanaita hali hii *tathmini ya ukubalifu.*

Lugha ya Kiswahili huleksisha kipengele cha lengo la kitendo sogezi katika vipashio kama nomino, KN, KE na KH.

#### 2.2.4.1 Maelezo ya Lengo kwa kutumia Nomino na KN

Lengo huweza kuleksishwa ndani ya nomino au kuelezwa kwa KN katika Kiswahili. Kwa mfano:

41) *Musa alimrushia <u>Hamisi</u> mpira*.

Katika sentensi hii, *Hamisi* ndiye Lengo la Kitendo sogezi husika.

42) *Mwendawazimu aliwarushia <u>wanafunzi na walimu</u> mawe*. (KN)

#### 2.2.4.2 Maelezo ya Lengo kwa Kutumia Kielezi au KE

Lengo vilevile huweza kuelezwa kwa kutumia kielezi au KE katika lugha ya Kiswahili. KE husika kinaweza kuwa cha neno moja au zaidi. Kwa mfano:

43) *Mbayuwayu wanaelekea <u>nyumbani</u>*.

Katika sentensi hii, lengo la usogezi ni *nyumbani.*

### 2.2.4.3 Maelezo ya Lengo kwa Kishazi kitegemezi

Vipo vishazi vitegemezi ambavyo vinarejelea mahali ambapo kitendo fulani kinatendeka. Vishazi hivi vinaweza kutumika kama lengo la kitendo sogezi. Kwa mfano:

44) *Mvulana alifika alipokuwa mbwa*.

### 2.2.5 Msingi-pitwa

Hoffman (2011:19) anaeleza kwamba msingi-pitwa ni msingi ambao si mwanzo wa usogezi wala mwisho wake bali upo sehemu fulani katika njia kati ya chanzo na lengo. Kwa hivyo, katika kusonga kwake, umbo huupita msingi-pitwa katika sehemu fulani likiwa njiani kuelekea kwa lengo (ambalo linaweza kutajwa au lisitajwe). Hata hivyo, msingi-pitwa lina umuhimu tu unapotumiwa kueleza kitendo sogezi husika. Sentensi zifuatazo zinaonyesha kitendo sogezi kinachohusu Msingi-pitwa. Kwa mfano:

45) *Babu amelipita lile jiwe jeupe*.

46) *Gari letu zee limelipiku lao jipya*.

Sentensi hizo za hapo juu zinadhihirisha kuwa Msingi-pitwa (sehemu iliyopigiwa mstari) unaweza kuwa umetuwama au unasonga pia katika mwelekeo sawia na ule wa umbo husika au liwe linasonga kuelekea upande tofauti na wa umbo linalorejelewa. Kwa mfano:

47) *Gari letu limepitana na lao*.

Sawa na ilivyo na chanzo na lengo, msingi-pitwa huweza kuelezwa kwa kutumia nomino, kielezi, KE na kishazi kitegemezi.

### 2.2.6 Kisababishi

Kisababishi hurejelea kile kitu kinachosababisha umbo kusonga kutoka sehemu moja hadi nyingine. Kwa hivyo, kisababishi sharti kiwe na uwezo fulani wa kulifanya Umbo kusonga. Kisababishi huweza kuwa binadamu, wanyama, upepo au hata maji. Kwa mfano:

48) <u>Kitwana</u> *amesukuma rukwama hadi nyumbani*.

49) <u>Upepo</u> *unapeperusha matawi ya miti angani*.

50) <u>Maji</u> *yameisomba mimea yetu*.

Visababishi katika sentensi hizi ni *Kitwana*, *upepo* na *maji*. Kwa hivyo, ni dhahiri kuwa kipengele hiki huelewa na nomino au KN katika lugha ya Kiswahili.

## 2.3 Vitenzi vya Usogezi

Lugha ya Kiswahili ina vitenzi kadha vinavyotumiwa na watumiaji wake kueleza vitendo sogezi. Hivi ni vitenzi vya aina maalumu kwa kuwa, tofauti na vitenzi vingine, hubeba maana ya usogezi. Talmy (2000a) anaeleza kuwa vitenzi vya usogezi hubeba maana ya usogezi katika mizizi yao. Noonan (2003) anaeleza kuwa vitenzi ambavyo havina usogezi katika maana yao ya kimsingi haviwezi kutokea pamoja na maelezo yoyote ya njia ila tu iwapo kitenzi cha usogezi kinacholeksisha njia kinapotumika kama kitenzi kikuu katika utungo husika. Vitenzi vya usogezi, kimsingi, ni vitenzi ambavyo hubeba maana ya usogezi katika mizizi yao. Kwa hivyo, vitenzi vya usogezi huwa na maana ya usogezi katika maana zao za kileksia. Hali hii inadhihirisha kuwa maana ya usogezi ni sehemu aushi ya maana ya vitenzi husika na kuwa maana hiyo haiwezi kutenganishwa na mzizi wa kitenzi husika. Mnato kati ya mzizi wa kitenzi cha usogezi na maana ya usogezi hauwezi kuvunjwa kwa namna yoyote ile. Matumizi ya vitenzi hivyo, kimsingi, humaanisha kuwa kuna usogezi fulani unaotendeka. Kimsingi, kitenzi cha usogezi hubeba maana mbili katika mzizi wake. Maana hizo (muundo wa kisemantiki wa vitenzi hivyo vya usogezi) zinaweza kujitokeza kwa namna zifuatazo:

a) KITENZI [usogezi+njia] Kwa mfano: *toka*, *enda* na *ondoka*.

b) KITENZI [usogezi + namna] Kwa mfano: *tembea*, *kimbia* na *ruka*.

c) KITENZI [usogezi + umbo] Kwa mfano: *nyesha*

Kwa hivyo, tunaweza kuwa na vitenzi vya usogezi vya njia au vitenzi vya usogezi vya namna. Vitenzi vya usogezi vinavyoleksisha umbo ni vichache mno katika Kiswahili. Hapa nimetambua kimoja tu jinsi nilivyoonyesha hapo juu. Hata hivyo, vitenzi vya usogezi vya njia na vile vya namna huwa kadha katika Kiswahili. Vilevile, kuna wataalamu ambao wamependekeza aina nyingine ya vitenzi vya Usogezi viitwavyo vitenzi vya usogezi vya usonde. Vitenzi hivi hueleza Usogezi kwa kurejelea mwelekeo

wa msemaji. Vitenzi vya usonde ni kama vile *njoo, kuja, enda* na *rudi.* Nitavishughulikia vitenzi hivi baadaye katika tasnifu hii.

Mateu & Matellan (2012) wanaeleza kuwa matumizi ya vitenzi vya usogezi huathiriwa na kanuni za kisintaksi zilizomo katika lugha husika. Kwa hivyo, ni kanuni hizi zinazoathiri namna lugha itakavyotumia vitenzi vya njia na vya namna. Zwarts (2004) anamnukuu (Cruse 1986) ambaye anaeleza kuwa vitenzi vya usogezi vinaweza kuwa vinyume vya vitenzi vingine vya usogezi kwa namna mbalimbali. Kimsingi, vitenzi vya usogezi vya Kiswahili pia vinaweza kuwa vinyume vya vingine katika mwelekeo wa usogezi inavyoonekana katika jozi za vitenzi hivi: *ingia-toka, tumbukia-ibuka, shuka-panda* na *enda-rudi*. Ni vyema kutambua kwamba vitenzi hivi hutegemeana katika kueleza vitendo sogezi. Tunaelewa maana ya *shuka* kwa kuwa tunajua maana ya *panda*. Kwa mfano, ili umbo *litoke* ndani ya msingi fulani sharti kwanza liwe *liliingia* au *limeingia* ndani ya Msingi huo husika. Vivyo hivyo, ili umbo *lishuke* sharti kwanza *lipande*.

Kuna vitenzi vingine vya usogezi ambavyo hudhihirisha kinyume ndani yao. Vitenzi hivi havina vitenzi ambavyo ni vinyume vyao. Hali ya kinyume inatokea ndani ya kitenzi kile kile kimoja. Mifano ya vitenzi kama hivi ni *zunguka, ruka, vuka* na *pita*.

### 2.3.1 Sifa za Vitenzi vya Usogezi

Cardini (2008) anatoa sifa mbalimbali za vitenzi vya usogezi. Ninakubaliana na maoni yake kwamba ili kitenzi kiweze kufuzu kuwa kitenzi cha usogezi, ni sharti kiwe na sifa zifuatazo:

a) **Maana ya kitenzi husika lazima ionyeshe wazi badiliko la kimahali**.

Kwa kuwa usogezi huhusu badiliko la kimahali, ni badiliko hilo ndilo huleta tofauti kati yake na hali ya kutulia/kutuwama mahali. Hata hivyo, ili kuhakikisha kuwa kipengele hiki cha kisemantiki kinakuwa sifa muhimu ya maana ya vitenzi, kuna matakwa fulani ambayo sharti yatimizwe.

Kwanza kabisa, maana ya badiliko la kimahali sharti ielezwe katika mzizi wa kitenzi husika bali si kwa viambishi au maneno yanayokifuata kitenzi husika. Kwa mfano:

51) *Bundi ametoka ndani ya shimo na kumwangalia mvulana*.

Katika sentensi hii, mahali alipokuwa bundi kabla ya usogezi ni *ndani ya shimo*. Kwa hivyo anaposonga anaelekea nje. Maana ya usogezi huu imo ndani ya mzizi wa kitenzi *toka*.

Pili, kipengele cha usogezi sharti kipewe umulikaji wa moja kwa moja na wa kimsingi katika maana ya kitenzi husika. Kwa hivyo, vitenzi ambavyo huonyesha usogezi kwa njia isiyokuwa ya moja kwa moja haviwezi kuwa vya usogezi kwa sababu umulikaji wao wa moja kwa moja na wa kimsingi umewekwa kwa kipengele kingine. Kwa mfano, kitenzi kama *winda* (kutafuta mnyama kwa lengo la kumuua) kinarejelea usogezi wa namna fulani lakini si cha usogezi kwa kuwa hakielezi usogezi moja kwa moja na kuupa umulikaji wa msingi. Kwa mfano:

52) *Wavuvi walilivuka ziwa wakivua samaki*. (Umulikaji wa msingi upo kwenye usogezi)

53) *Msasi anawinda sungura msituni*. (Umulikaji wa msingi haupo kwenye usogezi)

**b) Maana ya kitenzi husika sharti ihusu Usogezi hamishi**

Ni wazi kuwa ni usogezi hamishi tu ndio unaoweza kuwa na vipengele vyote ambavyo Talmy anaviorodhesha kama vipengele vya vitendo sogezi. Kwa hivyo, kitenzi kama *inama* au *chutama* si vya usogezi kwa kuwa havirejelei uhamisho wowote wa umbo kutoka sehemu moja hadi nyingine bali hurejelea badiliko la mkao wa mwili wa mtu katika sehemu ileile moja.

Kwa kuzingatia sifa hizi, vitenzi vya lugha ya Kiswahili sanifu ambavyo ninavichukulia kuwa vya usogezi humu ni kama vilivyomo katika mifano ya hapa chini:

54) *Mwendawazimu anakimbia barabarani*.

55) *Wavamizi wengi waliu<u>vuka</u> Mto Tana.*

56) *Chura ame<u>chupa</u> hadi majini.*

57) *Wachezaji wame<u>fika</u> kutoka uwanjani*.

Katika mifano ya hapo juu, kila kitenzi kilichopigiwa mstari kinarejelea kusonga kwa umbo kutoka sehemu moja (chanzo) hadi sehemu nyingine (lengo).

Levin (1993) anaviainisha vitenzi vya usogezi kwa aina mbalimbali huku akizingatia kigezo cha kisemantiki, yaani maana za vitenzi hivyo. Uanishaji wake ni kama ufuatao:

a) Vitenzi vya usogezi unaoelekezwa kama vile *fika, enda* na *kuja*

b) Vitenzi vya namna ya usogezi kama vile *bingiria, kimbia, elea, dunda* na *ruka*

c) Vitenzi vya namna ya usogezi kwa kutumia gari kama vile *endesha.*

d) Vitenzi vya kufukuza kama vile *fukuza*, *fuata* na *kimbiza*

e) Vitenzi vya kuandama kama vile *andama* na *sindikiza*

Katika sehemu inayofuata, ninafafanua zaidi kuhusu vitenzi hivi na kueleza namna vinavyohusika katika maelezo ya usogezi katika Kiswahili sanifu. Ninazingatia vilevile, jinsi vitenzi hivi vya usogezi vinavyohusiana na vipengele vingine vya usogezi, yaani umbo na msingi (chanzo na lengo).

### 2.3.2 Aina za Vitenzi vya Usogezi: Matumizi na maana

Katika utafiti huu, nitautumia uanishaji alioutumia Levin (keshatajwa). Uainishaji huu umefanywa kwa msingi wa kisemantiki. Hata hivyo, nitaufanyia mabadiliko machache ili kuhakikisha vitenzi vyote vya usogezi katika Kiswahili sanifu vimeainishwa katika angalau aina moja. Ninaeleza vilevile jinsi vitenzi vya kila aina vinavyohusiana na vipengele vya chanzo na lengo. Ninaviainisha vitenzi vya usogezi katika lugha ya Kiswahili kwa aina sita ninavyoonyesha hapa chini.

### 2.3.2.1 Vitenzi vya Usogezi Unaoelekezwa

Vitenzi vya usogezi unaoelekezwa ni vitenzi vinavyoleksisha kipengele cha Njia katika mizizi yao. Vitenzi hivi hudhihirisha njia ya usogezi katika maelezo ya kitendo sogezi. Nimeorodhesha vitenzi vifuatavyo katika aina hii: *njoo, kuja, enda, panda, shuka, paa, tumbukia, ibuka, toka, elekea, fika, toma, vuka, ondoka, ingia, kimbilia* na *rukia*. Nitavishughulikia vitenzi vya *njoo, kuja* na *enda* kwa tafsili baadaye katika utafiti huu nitakaposhughulikia swala la usonde.

Jambo moja lililo wazi kuhusu vitenzi hivi vya usogezi ni kuwa vinategemea sana kuhusishwa kwa chanzo au lengo ama vyote viwili kila vinapotumiwa. Ninadhihirisha hali hii kwa kutumia sentensi zifuatazo:

58) *Mwokoaji ametumbukia majini*.

59) *Mifugo wanaelekea malishoni*.

60) *Ndege ametoka katika kiota chake*.

Baadhi ya vitenzi vya aina hii hueleza mwelekeo wa kuingia ndani ya kitu au kutoka ndani ya kitu. Si lazima kitu hicho kiwe kinafunika umbo gubigubi. Linaweza kuwa wazi tu kama *uwanja*. Kwa mfano:

61) *Wachezaji wametoka uwanjani*.

### 2.3.2.2 Vitenzi vya Namna ya Usogezi

Vitenzi vilivyomo katika aina hii ya vitenzi vya usogezi hubeba maana ya usogezi na namna ya usogezi huo katika mizizi yao. Kwa hivyo, kimsingi vitenzi vya namna ya usogezi havileksishi kipengele cha njia katika mizizi yao. Hivyo basi, kwa kuwa kipengele cha njia ni cha lazima katika maelezo ya kitendo sogezi, sharti vitenzi hivi vifuatwe na vitenzi au vifuatilizi ambavyo vinaeleza njia. Vitenzi vya usogezi vilivyomo katika aina hii ni pamoja na *bingiria, kimbia, elea, dunda, ruka, tiririka, tembea, zurura, fululiza,* na *chupa*. Kwa mfano:

62) *Mhadhiri alitembea hadi darasani*.

63) *Matawi ya miti yanaelea majini*.

Hata hivyo, kuna wakati ambapo vitenzi vinavyoeleza namna ya usogezi vinapotumiwa, kipengele cha njia hakidhihiriki wazi katika vipashio vya kileksia au vya kisintaksia. Kwa mfano:

64) *Mwanaharusi alitembea haraka jana jioni*.

*Mwanaharusi* [umbo] *alitembea* [usogezi + namna] *haraka* [namna] *jana jioni*.

Ingawa kipengele cha njia hakidhihiriki wazi katika sentensi hii, bado itaeleweka kwa msikilizaji kuwa usogezi unaorejelewa ulitendeka katika njia fulani kwa kuwa kipengele cha njia hakiwezi kukosekana katika kitendo sogezi.

**2.3.2.3 Vitenzi vya Namna ya Usogezi kwa kutumia chombo**

Vitenzi vya aina hii huhusisha usogezi ambapo umbo hubebwa ndani ya chombo kingine kinachosonga. Katika Kiswahili sanifu, vitenzi vya aina hii huwa vichache. Nimetambua viwili tu katika utafiti huu. Vitenzi husika hapa ni kama *endesha* na *safiri*. Kwa mfano:

65) *Abiria wanasafiri kwa gari zuri sana*.

*Abiria* [umbo] *wanasafiri* [usogezi + njia] *kwa gari zuri sana* [namna].

Katika sentensi hii, umbo (abiria) linasonga lakini likiwa ndani ya chombo (gari zuri sana).

**2.3.2.4 Vitenzi vya Usababishi**

Kimsingi vitenzi vya usababishi hurejelea Usogezi ambao husababishwa au kuchochewa na kitu kingine. Kwa hivyo, umbo linasonga kwa sababu limefanyizwa kusonga na kisababishi. Tukio la kusonga kwa umbo ni tokeo la athari au tendo la kisababishi. Vitenzi hivi vinapotumiwa kueleza kitendo sogezi, hivyo basi, sharti kipengele cha kisababishi kiwapo hata kama hakijadhihirika kisintaksia. Mifano ya vitenzi hivi ni kama vile *vuta, sukuma* na *angusha.* Kwa mfano:

*66) Mbwa ameangusha mzinga wa nyuki.*

Vitenzi vya usogezi *vuta* na *sukuma* ni vya kipekee katika aina hii ya vitenzi. Vitenzi hivi vinapotumiwa, tunapata kuwa kitendo sogezi kinachorejelewa huweza kuwa na maumbo mawili. Kwa mfano:

*67) Mfanyakazi anasukuma rukwama.*

Katika sentensi hii, *Mfanyakazi* anasababisha *rukwama* kusonga lakini naye anasonga vilevile. Kule kusukuma rukwama kunatendeka kwa mfululizo. Kuna hali ya mshikamano unaojitokeza kati ya mfanyikazi na rukwama hivi kwamba moja ikisonga na nyingine inasonga vilevile. Kwa hivyo, mfanyikazi anaonekana kuwa na majukumu mawili, yaani umbo na kisababishi. Umbo kwa kuwa anasonga na kisababishi kwa kuwa anasababisha *rukwama* kusonga. Tunaweza kusema kuwa ana majukumu kuwili- kusonga na kusababisha kitu kingine kusonga.

Hata hivyo, kuna wakati ambapo kitenzi cha usogezi huhusisha Kisababishi kilichotuwama tu. Kwa mfano:

68) *Ndovu amelisukuma jiwe likabingiria mlimani*.

Hapa *ndovu* ni kisababishi tu bali hasongi pamoja na *jiwe* wakati *jiwe* linaposonga.

Kitenzi cha usogezi *vuta* kinamaanisha kuwa kuna maumbo mawili yanayosonga kwa wakati mmoja- linalovuta na linachovutwa. Kwa mfano:

69) *Mfugaji anamvuta mbuzi kuelekea malishoni*.

Hata hivyo, kuna wakati ambapo kinachovuta si umbo kwani hakisongi kama kinachovutwa. Kwa mfano:

70) *Kamau anamvuta ng'ombe wake*.

Katika sentensi hii, *Kamau* anaweza kuwa anasonga au amesimama na labda anadhamiria kuleta *ng'ombe* karibu naye.

Kwa kuzingatia mwelekeo wa usogezi wa umbo, kitenzi cha usogezi *sukuma* kinadhihirisha usogezi unaoelekea mbele huku kitenzi cha usogezi *vuta* kikiweza kuonyesha mwelekeo wa mbele au nyuma. Kitenzi cha angusha hakidhihirishi upande au mwelekeo wa Kitendo sogezi chenyewe.

#### 2.3.2.5 Vitenzi vya Kuandama

Kiswahili sanifu kina vitenzi vichache vya usogezi vya aina hii. Katika utafiti huu nimeweza kutambua vitano tu – *andama, fuata, fukuza, kimbiza* na *sindikiza*. Kimsingi vitenzi hivi vya usogezi hutumiwa kueleza kitendo sogezi kinachohusisha kusonga kwa vitu viwili au zaidi kwa usambamba fulani. Vitenzi hivi vinaweza kutumiwa kueleza usogezi wa maumbo mawili au zaidi yanayoelekea upande mmoja. Kwa mfano:

71) *Mama amewasindikiza wageni mjini*.

Katika sentensi hii, *mama* na *wageni* ni maumbo kwa kuwa wote wanasonga kuelekea upande mmoja kwa wakati mmoja na bila mmoja wao kusababisha mwingine kusonga.

Hata hivyo, vitenzi vya usogezi *andama, fuata, fukuza* na *kimbiza* vinapotumiwa, basi umbo linalohusika linasonga kuelekea kwa lengo ambalo pia linasonga kutokana na ile hali kuwa umbo linaliendea. Kwa mfano:

72) *Simba anamfukuza sungura mbugani*.

*Simba* [umbo] *anamfukuza* [usogezi+namna] *sungura* [lengo] *mbugani* [msingi].

#### 2.3.2.6 Vitenzi vya Mpitano

Vitenzi vya mpitano hutumiwa kueleza usogezi unaohusu vitu viwili. Vitenzi hivi huwa ni viwili katika Kiswahili sanifu - *piku* na *pita*. Kitenzi cha usogezi *piku* hutumika kueleza kitendo sogezi ambacho kinahusisha vitu viwili vinavyosonga kuelekea kwa upande mmoja. Hata hivyo, kimoja ambacho mwanzo kilikuwa nyuma, kinazidi kasi kile kilichokuwa mbele yake. Kwa namna hii, kilichokuwa nyuma kinakuwa mbele na kilichokuwa mbele kinakuwa nyuma. Kile ambacho kimekipiku kingine ndicho umbo huku kilichopikuliwa kikiwa Msingi-pitwa. Kwa mfano:

*73) Basi la Nya-Ugenya limelipiku lile la Matunda.*

*Basi la Nya-Ugenya* [umbo] *limelipiku* [usogezi+njia] *lile la Matunda* [lengo].

Hizo ndizo aina za vitenzi vya usogezi katika Kiswahili sanifu. Vitenzi hivi vinapotumiwa na wazungumzaji wa Kiswahili sanifu, huweza kuwa na mahitaji mbalimbali ya Kisintaksia. Kuna vile vitenzi vya usogezi ambavyo vikitumiwa basi sharti umbo, chanzo, msingi-pitwa

au lengo lidhihirike wazi katika vipengele vya kisintaksia katika sentensi husika. Vilevile, uambishaji wa vitenzi hivi katika kauli mbalimbali huweza kubadilisha mahitaji hayo katika sentensi.

## 2.4 Muhtasari

Katika sura hii, nimeshughulikia namna vipengele vya vitendo sogezi umbo, usogezi, chanzo, msingi-pitwa, lengo na kisababishi vinavyoelezwa kwa kutumia vipashio vya kileksia na kisintaksia katika lugha ya Kiswahili. Vilevile, nimedhihirisha aina mbalimbali za vitenzi vya usogezi na uainishaji wao kisemantiki. Pia nimetoa mifano mbalimbali ya sentensi zinazodhihirisha jinsi vipengele hivi vinavyojitokeza katika lugha ya Kiswahili. Vipengele vya usogezi, namna na njia, vinashughulikiwa katika sura mbili zinazofuatia.

## SURA YA TATU

## 3.0 MAELEZO YA NAMNA KATIKA KISWAHILI

### 3.1 Utangulizi

Katika sura ya pili, nimeshughulikia vipengele vinne vya vitendo sogezi na maelezo yao katika Kiswahili sanifu. Vipengele ambavyo nimevishughulikia tayari ni umbo, Msingi (chanzo, lengo na msingi-pitwa) na kisababishi. Vilevile, nimevishughulikia vitenzi vya usogezi na aina zake.  Katika sura hii, ninaangalia jinsi kipengele cha namna kinavyoelezwa kwa kutumia vipashio mbalimbali katika Kiswahili sanifu. Kiswahili sanifu kinadhihirisha matumizi ya vipashio mbalimbali kueleza namna ya vitendo sogezi. Ninashughulikia kila kipashio kinachohusika na kukitolea mifano ya matumizi yake katika sentensi za Kiswahili sanifu.

### 3.2 Namna katika Kiswahili Sanifu

Nilivyotaja awali, namna ni kipengele ambacho ni cha hiari katika maelezo na masimulizi ya vitendo sogezi. Lugha ya Kiswahili hueleza dhana ya namna ya usogezi katika mizizi ya vitenzi vya usogezi pamoja na vifuatilizi. Kuna idadi fulani ya vitenzi vya usogezi vinavyoleksisha maana ya namna ya usogezi katika mizizi yao. Mizizi ya vitenzi hivyo huwa na maana ya usogezi na namna kwa pamoja. Kwa hivyo, huonyesha kuwa usogezi ulitendeka, unatendeka au utatendeka na namna ya kutendeka kwake. Vilevile, kuna aina nyingine ya maneno kama vile vielezi, vihusishi na tungo kama vile virai na vishazi ambavyo hueleza kipengele cha namna ya kutendeka kwa kitendo sogezi katika Kiswahili sanifu. Hata hivyo, kuna mara kadha ambapo kipengele cha namna ya usogezi hakielezwi katika sentensi za Kiswahili sanifu hasa wakati ambapo namna ya usogezi si muhimu kwa mawasiliano husika. Hali hii ninaiita, katika utafiti huu, namna isokuwepo.

#### 3.2.1 Namna katika Vitenzi

Kuna vitenzi vya Kiswahili ambavyo hueleza namna ya usogezi. Katika vitenzi hivyo, namna ya kutendeka kwa kitendo sogezi huelezwa katika mizizi. Kimsingi, vitenzi husika huwa na nafasi moja wazi ya kubebea maana ya namna kwa kuwa njia inaelezwa katika kifuatilizi. Kwa hivyo, vitenzi hivi vya namna vinapotumiwa katika sentensi, mara nyingi hufuatwa na

kipashio kingine kilicho na sifa ya kuwa kifuatilizi kinachobeba maana ya njia. Vitenzi vya usogezi vinavyoeleza namna hueleza namna za aina mbalimbali kama vile mtindo wa kusonga na kasi ya kusonga. Vitenzi vya usogezi vinavyoeleza namna katika mizizi yao huwa na muundo ufuatao wa kisemantiki:

Kitenzi [usogezi+namna]

Kwa mfano:

74) *Pipa linabingiria mlimani*.

*Pipa* [umbo] *linabingiria* [usogezi+namna] *mlimani* [msingi].

Tunaweza kupima ikiwa kitenzi ni cha namna kwa kuangalia iwapo kitenzi hicho kinapotumiwa pekee katika sentensi basi mwelekeo wa usogezi unabaki bila kuelezwa. Kwa mfano, umbo linaweza *kupaa, kukimbia, kutembea* au *kubingiria* bila kuonyesha mwelekeo maalumu. Kipengele cha namna kinajibu swali la "Vipi?" bali si "Wapi?"

Ninaviorodhesha vitenzi vya usogezi husika hapa chini kwa kuzingatia aina za Namna vinavyozieleza.

### 3.2.1.1 Vitenzi Vya Usogezi vya Namna ya Kasi

Mojawapo ya aina za namna inayoelezwa na vitenzi vya usogezi katika lugha ya Kiswahili ni mwendo au kasi ya usogezi wa umbo. Kwa hivyo, vitenzi hivi hurejelea vipimo vya kasi ya usogezi wa umbo. Vipimo hivyo vya kasi huwa ni vya jumla tu bali si mahususi. Vitenzi vya usogezi haviwezi kueleza kasi mahususi ya usogezi. Kwa mfano:

75) *Mbwa anakimbia kuelekea mtoni*.

*Mbwa* [umbo] *anakimbia* [usogezi + namna] *kuelekea* [usogezi + njia] *mtoni* [lengo].

Katika sentensi hii, kitenzi *kimbia* kimebeba maana ya usogezi na ile ya namna. Usogezi unatendeka vipi? Kwa *kukimbia*. Maana ya sentensi hii inatofautiana na maana ya hizi mbili zinazofuatia kwa sababu ya tofauti ya kasi ya kusonga kwa Umbo la Kitendo sogezi.

76) *Mbwa anatembea kuelekea mtoni.*

*Mbwa* [umbo] *anatembea* [usogezi + namna] *kuelekea* [usogezi + njia] *mtoni* [lengo].

au

77) *Mbwa ananyapianyapia kuelekea mtoni*.

*Mbwa* [umbo] *ananyapianyapia* [usogezi + namna] *kuelekea* [usogezi + njia] *mtoni* [lengo].

Kasi inayorejelewa na vitenzi hivi vitatu hutofautiana kwa viwango.

### 3.2.1.2 Vitenzi vya Usogezi vya Namna ya Mtindo wa Kusonga

Lugha ya Kiswahili vile vile ina vitenzi vya usogezi ambavyo hueleza kuhusu mtindo wa kusonga kwa umbo. Vitenzi hivi hurejelea hasa kile kinachotendekea mwili wa umbo wakati linaposonga. Umbo linaweza *kuyumbayumba*, *kuchechemea*, au *kutangatanga*. Kwa mfano:

78) *Gari linayumbayumba barabarani*.

*Gari* [umbo] *linayumbayumba* [usogezi + namna] *barabarani* [msingi].

79) *Nyoka anatambaa sakafuni*.

*Nyoka* [umbo] *anatambaa* [usogezi + namna] *sakafuni* [msingi].

Sentensi hii inaonyesha kuwa umbo linasonga lakini kwa mtindo fulani mahususi.

### 3.2.1.3 Vitenzi vya Usogezi vya Namna ya Urudiaji

Lugha ya Kiswahili vilevile, huweza kuonyesha namna ya kutendeka kwa kitendo sogezi kwa kurudia kitenzi kilekile kinachotaja kitendo sogezi husika. Kurudia neno huko kutamaanisha kuwa namna ya kufanya kitendo sogezi husika ni ziadi ya mara moja. Kutokana na hali hii, maana ya namna iliyomo katika kitenzi *tembea* ni tofauti na maana ya kitenzi *tembeatembea*. Kwa mfano:

80) *Kamau anatembea uwanjani*.

*Kamau*[umbo] *anatembea* [usogezi + namna] *uwanjani* [msingi].

81) *Kamau anatembeatembea uwanjani*.

*Kamau* [umbo] *anatembetembea* [usogezi + namna] *uwanjani* [msingi].

Katika sentensi ya pili, umbo limekuwa likirudia au kutenda usogezi husika kwa muda mrefu au kwa njia ya kuchusha au kwamba usogezi husika hauna mwelekeo mahususi.

### 3.2.1.4 Vitenzi vya Usogezi vya Namna ya kuingia katika Lengo


Vitenzi vya usogezi vya aina hii huleksisha namna inayohusu jinsi umbo linavyingia katika lengo. Vitenzi vilivyomo hapa ni kama vile *toma* na *tumbukia*. Kwa mfano:

82) *Kamama aliji<u>toma</u> chumbani akihema*.

*Kamama* [umbo] *alijitoma* [usogezi+ namna (kwa kasi na ghafla)] *akihema*.

Hata hivyo, ni vizuri kukumbuka kuwa hiki kitenzi cha *toma* kinaweza kubeba kipengele cha njia vilevile. Tunaposema kuwa umbo *limejitoma* ndani ya lengo fulani, kimsingi tunaonyesha kuwa mwelekeo wa usogezi ni wa kuingia ndani ya lengo. Inavyoonekena, kitenzi *toma* kina maana ya *ingia ghafla* au *ingia kwa haraka*. Kwa hivyo *toma* ni mojawapo ya vitenzi vya Kiswahili ambavyo vinaonyesha uwezo wa kuleksisha vipengele vya usogezi, njia na namna katika mzizi wake. Kwa hivyo, ninaweza kusema kuwa kitenzi *toma* huwa na muundo wa kisemantiki ufuatao:

*toma* [usogezi+ njia (ingia ndani ya) + namna (ghafla/haraka)]




*Mchoro 1*: *Muundo wa Kisemantiki wa kitenzi <u>toma</u>.*

Vitenzi vingine vinavyodhihirisha muundo kama huu ni pamoja na *fyatuka, kurupuka* na *chomoka*.

#### 3.2.1.5 Vitenzi vya Usogezi vya Namna ya kutoka katika Chanzo

Vitenzi hivi hurejelea namna ambavyo umbo linatoka katika chanzo. Kwa hivyo, vitenzi vinavyohusika hapa hutumika tu wakati ambapo usogezi unahusu umbo linalotoka katika chanzo. Kwa mfano, kitenzi *chomoka* kinatumika wakati ambapo mwelekeo wa usogezi unaelezwa kwa kurejelea chanzo cha kitendo sogezi husika. Hata hivyo, kitenzi hiki kinadhihirisha sifa sawa na zile za kitenzi *toma*. Kinaonyesha kuwa kinabeba maana ya usogezi, namna na njia kwa pamoja. Umbo linaposemekana *kuchomoka* sharti liwe lilikuwa ndani ya chanzo kisha likatoka ghafla kwa haraka. Kwa mfano:

83) *Panya amechomoka shimoni*.

*Panya* [umbo] *amechomoka* [usogezi + namna (toka ghafla) + njia (enda nje ya] *shimoni* [chanzo].

Kwa hivyo, kwa kurejelea vitenzi hivi vya usogezi, tunaona kuwa Kiswahili huleksisha kipengele cha namna katika vitenzi vyake. Kwa hivyo, Kiswahili kinaweza kuonekana kuwa ni lugha mfumbatio-kifuatilizi kwa kuwa vitenzi hivi vikitumiwa katika sentensi basi sharti kipengele cha njia kielezwe katika kifuatilizi. Hata hivyo, Kiswahili pia hueleza kipengele cha namna katika vipashio vingine tofauti na vitenzi jinsi ninavyoonyesha hapa chini.

### 3.2.2 Uleksishaji wa Namna katika Vifuatilizi

Lugha ya Kiswahili hueleza namna ya vitendo sogezi katika vifuatilizi. Vifuatilizi hivi huweza kuwa vielezi au KE ama vishazi vitegemezi. Ninavishughulikia vifuatilizi hivi hapa chini.

#### 3.2.2.1 Kielezi na Kirai Elezi (KE)

Aina ya kwanza ya vifuatilizi vinavyoleksisha namna ya vitendo sogezi ni kielezi na Kirai elezi (KE). Mgullu (1999), Myachina (1981) wanaeleza kuhusu vielezi vya Kiswahili na aina zake huku Massamba n.w (2001) wakieleza kuhusu KE. Vielezi na virai elezi husika huweza kuonyesha namna za aina mbalimbali. Kwa hivyo, namna hapa haijaleksishwa katika mizizi ya vitenzi vya usogezi bali katika KE. KE husika sharti kitanguliwe na kitenzi cha usogezi katika sentensi. Kwa hivyo, vifuatilizi hivi huongeza tu maana kwa kitendo sogezi ambacho tayari kimetajwa na kitenzi katika sentensi hiyo moja. Kielezi na KE huweza kueleza kuhusu namna za kasi ya umbo au mtindo wa usogezi husika.

#### 3.2.2.1.1 Kasi ya Usogezi wa Umbo

Kasi ya usogezi huweza kuelezwa kwa kutumia kielezi au KE katika lugha ya Kiswahili.

Kwa mfano:

84) *Mbwa na swara wanakimbia* <u>*haraka sana*</u>.

*Mbwa na swara* [umbo] *wanakimbia* [usogezi + namna] *haraka sana* [namna]

Vielezi na KE sawa na vitenzi vya usogezi hueleza kasi ya jumla tu, yaani isiyokuwa mahususi.

#### 3.2.2.1.2 Mtindo wa Usogezi wa Umbo

Vielezi na KE huweza pia kueleza mtindo wa usogezi wa umbo katika kitendo sogezi. Mtindo wa kusonga kwa umbo unaweza kuhusishwa na mtindo wa kusonga kwa umbo jingine lisilokuwapo katika kitendo sogezi kinachorejelewa. Kwa mfano:

85) *Mwanamitindo anatembea* <u>*kitausi*</u>.

*Mwanamtindo* [umbo] *anatembea* [namna] *kitausi* [namna].

Katika kitendo sogezi kilichomo katika sentensi ya hapo juu, namna ya usogezi wa umbo unalinganishwa na mtindo wa kutembea kwa ndege aitwaye *tausi*. Kwa hivyo, ili msikilizaji aweze kuelewa maana ya kielezi hiki, ni sharti awe na ufahamu wa awali kuhusu mtindo wa kutembea kwa *tausi*. Sharti msikilizaji awe na picha fulani akilini ya ndege aitwaye *tausi* na mtindo wake wa kutembea ndiposa aelewe maana ya kielezi *kitausi*. Maana ya namna iliyomo katika kielezi hiki ni husishi. Mtindo huu wa kueleza namna ya usogezi kwa kutumia vielezi vya aina hii huwawezesha wazungumzaji wa Kiswahili kueleza namna mbalimbali kwa kuwa ni njia zalishi zaidi ya kuunda vielezi. Vielezi vya aina hii huweza kubuniwa kila wakati na kukubalika katika lugha. Mohamed (2001) anaviita vielezi hivi vielezi zalika kwa kuwa huundwa kutokana na maneno mengine.

Jambo la muhimu kukumbuka ni kuwa vielezi hivi huwa na chaguo la vitenzi vinavyovieleza. Hutumika tu pamoja na vitenzi fulani mahususi. Kwa mfano:

86) *Mtoto aliupanda mti kinyani.*

*Mtoto* [umbo] *aliupanda* [usogezi + njia] *mti* [msingi] *kinyani* [namna].

87) *Mbwa amechomoka kiswara.*

*Mbwa* [umbo] *amechomoka* [usogezi + njia + namna] *kiswara* [namna].

Hatuwezi kusema kuwa *Mbwa amechomoka kinyani* kwa kuwa *nyani* hawafahamiki kwa namna hiyo ya usogezi. Vivyo hivyo, hatuwezi kusema kuwa *Mtoto anakimbia kinyoka* kwa kuwa nyoka hakiimbii bali hutambaa.

Mifano zaidi ya vielezi vya aina hii ni kama vile *kikobe* na *kiduma.*

#### 3.2.2.2 Namna Vishazi vitegemezi

Lugha ya Kiswahili pia hueleza namna ya usogezi kwa kutumia vishazi vitegemezi. Sentensi husika huwa ni changamano na hivyo kuwa na kishazi huru na kishazi kitegemezi. Kitenzi cha usogezi kilichomo katika kishazi huru huweza kueleza njia au namna ya usogezi kisha kishazi kitegemezi kinachofuatia kiwe na kitenzi kinachoeleza namna ya usogezi unaotajwa na kile kitenzi cha kwanza cha njia au namna.

##### 3.2.2.2.1 Vitenzi viwili vya Namna

Katika hali hii, vitenzi vya namna vinatokea katika kishazi huru na kishazi kitegemezi katika sentensi changamano. Kwa mfano:

88) *Mgonjwa <u>anatembea</u> <u>akichechemea</u>.*

*Mgonjwa* [umbo] *anatembea* [usogezi + namna] *akichechemea* [usogezi + namna].

Katika sentensi hii, vitenzi *tembea* na *chechemea* vinatumika kueleza namna ya usogezi. Ile namna iliyomo katika *tembea* inaongezewa maana na namna iliyomo katika *chechemea*.

#### 3.2.2.2.2 Kitenzi cha Njia na Kitenzi cha Namna

Sentensi moja changamano inaweza kuwa na kitenzi kimoja cha njia na kingine cha namna. Kitenzi cha njia kinatokea katika kishazi huru huku kile cha namna kikitokea katika kishazi kitegemezi. Kwa mfano:

89) *Chura <u>anakuja</u> <u>akirukaruka</u>.*

*Chura* [umbo] *anakuja* [usogezi + njia] *akirukaruka* [usogezi + namna].

Kitenzi *kuja* kinaeleza usogezi na njia huku *rukaruka* kikieleza kuhusu namna ya usogezi.

### 3.2.2.3 Viigizi

Viigizi hurejelea hasa sauti zinazotolewa na umbo linaposonga. Mohamed (2001) anaeleza kuwa vielezi viigizi ni vile vielezi ambavyo huigiza milio ya matendo yanayotendwa. Hata hivyo, nimevieleza kando na vielezi vingine kwa kuwa matumizi yake huwa maalumu katika maelezo ya namna ya vitendo sogezi. Viigizi vinavyotumika katika Kiswahili kueleza Namna ya kitendo sogezi huhusu hasa sauti zinazotolewa na umbo likiwa katika chanzo, njia au likifika katika lengo. Kwa hivyo, Kiswahili kina viigizi vinavyohusiana na chanzo, msingi-pitwa na lengo la usogezi.

#### 3.2.2.3.1 Kiigizi katika Chanzo

Viigizi vinavyohusika hapa hueleza milio au sauti zinazotolewa na umbo linapoanza kusonga kuanzia chanzo. Kwa mfano:

90) *Nyuki walifyatuka fyu kutoka mzingani na kumfukuza mbwa*.

*Nyuki* [umbo] *walifyatuka* [usogezi + namna] *fyu* [namna] *kutoka* [njia] *mzingani* [chanzo] na *kumfukuza* [usogezi + njia] *mbwa* [lengo].

#### 3.2.2.3.2 Kiigizi katika Lengo

Viigizi vinavyotumika hapa hurejelea sauti zinazotolewa na umbo linapofika katika lengo. lengo linaweza kuwa ardhi, mchanga au maji. Kwa mfano:

91) *Mbwa anatumbukia majini chubwi!*

*Mbwa* [umbo] *anatumbukia* [usogezi + njia] *majini* [lengo] *chubwi* [namna]!

92) *Mbwa alitoka dirishani na kuanguka chini pu!*

*Mbwa* [umbo] *alitoka* [usogezi + njia] *dirishani* [chanzo] na *kuanguka* [usogezi + njia] *chini* [lengo] *pu* [namna]!

#### 3.2.2.3.3 Kiigizi katika Msingi-pitwa

Viigizi husika hapa hutumiwa hasa na vitenzi vya usogezi *pita* na *piku*.

*93) Gari lao lilitupita vu!*

*Gari lao* [umbo] *lilitupita* [usogezi + njia] *vu* [namna]!

#### 3.2.2.3.4 Kiigizi katika Njia

Viigizi vinavyoonyesha namna katika hali hii hueleza sauti au milio inayotokea umbo likiwa katika njia ya usogezi wake. Kwa mfano:

94) *Swara alikimbia kukurukakara akimbeba mvulana kichwani*.

*Swara* [umbo] *alikimbia* [usogezi + njia] *kukurukakara* [namna] *akimbeba mvulana kichwani*.

95) *Mdeni wangu alikuja mchakamchaka hadi kwangu*.

*Mdeni wangu* [umbo] *alikuja* [usogezi + njia] *mchakamchaka* [namna] *hadi* [njia] *kwangu* [lengo].

### 3.2.2.4 Kirai Husishi (KH)

Kipashio kingine ambacho huweza kueleza kipengele cha namna ya kitendo sogezi ni KH. KH hapa huweza kutoa maana ya namna inayohusiana na chombo cha usogezi, hisia iliyoandamana na usogezi husika au msukumo uliotumiwa katika usogezi huo. Ninatoa maelezo zaidi hapa chini.

#### 3.2.2.4.1 Chombo cha Usogezi

Hapa umbo linalosonga linakuwamo ndani ya chombo kingine ambacho kinasonga kutoka sehemu moja hadi nyingine. Kwa hivyo, umbo linasafiri ndani ya chombo hicho. Kwa mfano:

96) *Rais alisafiri kwa basi*.

*Rais* [umbo] *alisafiri* [usogezi + njia] *kwa basi* [namna].

Katika sentensi hii, *Rais* anasonga lakini kusonga kwake kunategemea kusonga kwa basi alililoliabiri.

#### 3.2.2.4.2 Hisia iliyoandamana na Kitendo sogezi

Katika maelezo haya ya namna ya usogezi kunaweza kuwapo na kisababishi ambacho ndicho kinachokuwa na hisia fulani kinaposababisha umbo kusonga au umbo lenyewe laweza kuwa na hisia fulani linaposonga. Kwa mfano:

97) *Mvulana alimwendea mbwa wake kwa huruma*.

*Mvulana* [umbo] *alimwendea* [usogezi + njia] *mbwa wake* [lengo] *kwa huruma* [namna].

98) *Mchezaji aliurusha mpira kwa hasira.*

*Mchezaji* [kisababishi] *aliurusha* [usogezi + njia] *mpira* [umbo] *kwa hasira* [namna].

#### 3.2.2.4.3 Nguvu au Msukumo Uliotumiwa katika Usogezi

Vihusishi vinavyohusika hapa hutoa maelezo kuhusu nguvu alizotumia kisababishi kulifanya umbo kusonga au nguvu zinazotumiwa na umbo katika kusonga kwake. Kwa mfano:

99) *Nyuki walimfukuza mbwa kwa fujo*.

*Nyuki* [umbo] *walimfukuza* [usogezi + njia] *mbwa* [lengo] *kwa fujo* [namna].

*100) Kamau aliruka kwa nguvu.*

*Kamau* [umbo] *aliruka* [usogezi + namna] *kwa nguvu* [namna].

### 3.2.2.4.4 Namna ya Kasi ya Usogezi wa Umbo

KH huweza vilevile kudhihirisha namna ya usogezi kwa kurejelea kasi ya umbo husika. KH huweza kuonyesha kasi ya viwango mahususi na ya jumla vilevile. Kwa mfano:

101) *Chura ametoka chupani <u>kwa haraka</u>.*

*Chura* [umbo] *ametoka* [usogezi + njia] *chupani* [chanzo] *kwa haraka* [namna].

102) *Gari linasonga <u>kwa kilomita mia kwa saa</u>.*

*Gari* [umbo] *linasonga* [usogezi + njia] *kwa kilomita mia kwa saa* [namna].

KH katika sentensi ya kwanza kinarejelea kasi ya jumla lakini KH katika sentensi ya pili kinarejelea kasi ya vipimo mahususi.

### 3.2.2.5 Maelezo ya Namna kwa Tashbihi

Lugha ya Kiswahili hutumia tashbihi mbalimbali kueleza namna ya usogezi wa kitendo sogezi. Maana ya namna iliyomo katika tashbihi husika ni lingashi kwa kuwa namna ya usogezi wa umbo inalinganishwa na namna ya usogezi wa umbo jingine lisilokuwapo katika kitendo sogezi kinachorejelewa. Kwa hivyo, jinsi ilivyo na vielezi vinavyobuniwa kutokana na nomino, ni sharti msikilizaji aelewe maana hasa ya awali kabla ya kuweza kuelewa maana iliyomo katika tashbihi inayohusika. Kwa mfano:

*103) Yehoshafati hutembea kama shujaa.*

*Yehoshafati* [umbo] *hutembea* [usogezi + namna] *kama shujaa* [namna].

104) *Farasi anakimbia haraka kama umeme*.

*Farasi* [umbo] *anakimbia* [usogezi + namna] *haraka kama umeme* [namna].

Tashbihi hizi za Kiswahili zinaweza kueleza aina mbalimbali za namna ya usogezi. Tashbihi huweza kuonyesha kasi ya usogezi au mtindo wa usogezi.

#### 3.2.2.5.1 Tashbihi zinazoonyesha Kasi ya Usogezi

Tashbihi zinazohusika hapa hutumia wanyama au vitu vinavyosonga kwa mwendo tofautitofauti na kuhusisha na mwendo wa umbo la kitendo sogezi husika. Kwa mfano:

105) *Mwanafunzi <u>anakimbia kama duma</u> akienda shuleni*.

*Mwanafunzi* [umbo] *anakimbia* [usogezi + namna] *kama duma* [namna] *akienda* [usogezi + njia] *shuleni* [lengo].

106) *Mzee Hamisi <u>anatembea polepole kama kobe</u>*.

*Mzee Hamisi* [umbo] *anatembea* [usogezi + namna] *kama kobe* [namna].

#### 3.2.2.5.2 Tashbihi zinazoonyesha Mtindo wa Usogezi

Tashbihi pia huweza kutumiwa kurejelea mtindo wa kusonga kwa umbo. Kwa mfano:

107) *Cheusi anatembea <u>akiyumbayumba kama mgonjwa</u>*.

*Cheusi* [umbo] *anatembea* [usogezi + namna] *akiyumbayumba* [usogezi + namna] *kama mgonjwa* [namna].

108) *Mwendawazimu <u>anatambaa kama nyoka</u>*.

*Mwendawazimu* [umbo] *anatambaa* [usogezi + namna] *kama nyoka* [namna].

Hapa mtindo wa kuyumbayumba kwa Cheusi unalinganishwa na anavyoyumbayumba mgonjwa huku kutambaa kwa mwendawazimu kukilinganishwa na kutambaa kwa nyoka.

### 3.2.2.6 Namna isiyokuwepo

Talmy (2000) anaeleza kuwa hivi vipengele vya vitendo sogezi vinaweza kuwekwa kwa vipashio vya nje (vya kileksia na kisintaksia) kwa njia tatu kuu. Mojawapo ya njia hizo ni uleksishaji ambayo tumeishughulikia katika mifano ya hapo juu. Njia ya pili anayoileza ni ile ya uhusishaji. Katika uhusishaji, msemaji anakosa kueleza kipengele fulani kwa kuwa kinaweza kueleweka kwa mlengwa kutokana na muktadha wa mawasiliano husika. Njia ya tatu anayoitaja ni ya udondoshaji. Katika udondoshaji, msemaji anaamua kutotoa maelezo fulani kwa kuwa si muhimu kwa wakati huo. Kwa mfano:

109) *Mvulana na mbwa wanatoka majini.*

*Mvulana na mbwa* [umbo] *wanatoka* [usogezi + njia] *majini* [chanzo].

110) *Papa ataondoka nchini leo jioni*.

*Papa* [umbo] *ataondoka* [usogezi + njia] *nchini* [chanzo] *leo jioni*.

Katika sentensi hizi mbili, msemaji haelezi namna ya usogezi wa umbo. Huenda ujumbe huo si muhimu kwa wakati huo. Kwa hivyo, hapa kipengele cha usogezi kinapewa kipaumbele zaidi.

Kutokana na maelezo na mifano ya hapo juu, ni wazi kuwa kipengele cha namna ya usogezi huweza kuwakilishwa kwa vipashio mbalimbali katika Kiswahili sanifu. Kwa hivyo, kipengele cha usogezi kilichomo ndani ya kitenzi cha usogezi kinaweza kuandamana na mojawapo ya vipashio hivyo ili kueleza namna ya kutendeka kwa kitendo sogezi. Kielelezo hiki kinachofuatia kinatoa muhtasari wa vipashio vinavyoeleza namna katika Kiswahili sanifu.

Usogezi + Namna

Kitenzi

Kitenzi cha Namna

KE

Viigizi

KH

Tashbihi

**3.2.2.7 Muhtasari**

Nimeweka wazi vipashio vinavyotumiwa kueleza namna ya usogezi katika lugha ya Kiswahili. Nimeorodhesha vipashio sita vinavyotumiwa kueleza namna katika Kiswahili sanifu na kutoa mifano muafaka ya sentensi ambamo vimetumiwa. Vipashio hivyo vinaeleza aina mbalimbali za namna ya usogezi. Ninashughulikia kipengele cha njia ya usogezi katika sura inayofuatia.

## SURA YA NNE

## 4.0 MAELEZO YA NJIA KATIKA KISWAHILI SANIFU

### 4.1 Utangulizi

Katika sura ya tatu nimeshughulikia maelezo ya namna ya usogezi ambayo yanaonyesha kuwa katika Kiswahili namna huelezwa kwa vitenzi vya usogezi, vielezi na KE, KH, tashbihi na viigizi. Kwa hivyo, nimesalia na kipengele cha njia ambacho ni muhimu katika kubainisha uainisho wa Kiswahili kulingana na vigezo vya Talmy. Hivyo basi, katika sura hii nitashughulikia jinsi njia inavyoelezwa katika Kiswahili sanifu. Itakavyobainika hapa, Kiswahili sanifu hueleza kipengele cha njia kwa kutumia vipashio mbalimbali tofauti na vitenzi vya usogezi. Hata hivyo, ninaanza kwa kutoa maelezo kuhusu kipengele hiki kabla ya kuonyesha jinsi kinavyoelezwa katika Kiswahili.

### 4.2 Maelezo

Talmy (1985) anaeleza njia kama mkondo unaofuatwa na umbo kwa kurejelea msingi. Slobin (1996) naye anasema kuwa njia ni usogezi hamishi wa umbo kutoka katika chanzo hadi katika lengo. Kwa hivyo, njia ni kipengele cha kitendo sogezi kinachorejelea njia inayofuatwa na umbo linaposonga kutoka katika chanzo likielekea katika Lengo lake. Njia hivyo basi, huwa kati ya chanzo na lengo.

Kipengele cha njia ni kipengele cha lazima katika kila kitendo sogezi. Kwa hivyo, kila kitendo sogezi sharti kiwe na kipengele cha njia kinachoelezwa kwa kutumia vipashio vilivyomo katika lugha husika. Hoja hii inaungwa mkono na Ibarretxe-Antunano (2004) anayemnukuu Slobin (2004:238) ambaye anaeleza kuwa kipengele cha njia ni cha lazima katika maelezo yote ya vitendo sogezi. Kwa hivyo, hatuwezi kusema kuwa lugha moja hueleza njia ya vitendo sogezi vyake huku nyingine ikikosa kufanya hivyo. Kila lugha sharti ikaeleze njia kwa namna moja au nyingine inapoeleza vitendo sogezi. Hapawezi kuwapo na kitendo sogezi bila ya njia kwa sababu umbo linalosonga sharti lifuate njia fulani. Hii ndiyo sababu Talmy aliweza kuainisha lugha za ulimwengu kwa aina mbili kwa kuzingatia zinapoleksisha kipengele cha njia.

Kipengele hiki ni tofauti na vipengele vya namna na kisababishi kwani hivi viwili ni vya hiari katika maelezo ya vitendo sogezi. Njia ni kipengele cha ndani katika kitendo sogezi ilhali namna na kisababishi vikiwa vipengele vya nje ya kitendo sogezi. Kutokana na hayo, Capelle na Declerk (2005) wanaeleza kuwa hata wakati ambapo njia haijaelezwa waziwazi katika sentensi, uwepo wake bado unaeleweka. Hivyo basi, ninaweza kusema kuwa kipengele cha njia huwa muhimu zaidi katika vitendo sogezi kuliko vya namna na kisababishi. Kwa namna nyingine, ninaweza kusema kuwa usogezi na njia ya usogezi huo zimo katika uhusiano usiotenganishika, yaani wa kijozi. Kwa hivyo, kila unapoeleza kitendo sogezi unalazimika kutaja njia yake vilevile. Hata hivyo, vipengele vya usogezi na njia huweza kuleksishwa katika vipashio tofauti. Jambo muhimu ni kuwa kimoja kikitokea na kingine sharti kiwepo pia. Landau & Zukowski (2003) wanamnukuu Jackendoff (1983) anayeeleza kuwa Njia hutekeleza jukumu muhimu sana katika kueleza vitendo sogezi katika lugha. Huwasaidia watumiaji wa lugha kujua hasa mwelekeo wa usogezi unaorejelewa.

Capelle & Declerk (keshatajwa) wanaongeza kuwa njia haielezwi moja kwa moja kila mara. Wanadhihirisha kuwa, kimsingi, ni sehemu moja tu au chache za Njia ndizo zinazoelezwa waziwazi kama vile umbo lake, lengo, chanzo na urefu wake. Kwa hivyo kulingana nao, njia huwa na vipengele mbalimbali ndani yake. Vipengele hivi, kulingana na maelezo yangu ya hapo awali, hudhihirika katika maelezo ya njia katika lugha ya Kiswahili pia.

Njia za usogezi huweza kuwa za aina mbalimbali. Jackendoff (1983:165) anatambua aina tatu za njia. Aina hizo ni njia funge, njia za mwelekeo na njia za mapitio. Aina hizi za njia pia hupatikana katika lugha ya Kiswahili kama ifuatavyo:

### 4.2.1 Aina za Njia za Usogezi

#### 4.2.1.1 Njia funge

Njia funge hurejelea kile ambacho Hoffman (2011) anataja kuwa njia za chanzo na njia za lengo. Ninachomaanisha hapa ni kuwa njia husika hapa ikirejelewa basi sharti chanzo au lengo pia litajwe katika sentensi husika. Kwa hivyo, njia funge ni ile ambayo imeshikamana au kufungamana na ama chanzo au lengo la usogezi.  Njia funge hutumia maneno kama

*kutoka, kuanzia* au *hadi* na *mpaka*. Vilevile, hutumia kiambishi tamati *-ni*. Katika aina hii ya njia, kirejelezi (chanzo au lengo) cha usogezi kimo ndani ya njia, yaani ni sehemu yake. Kwa mfano:

111) *Chura anapanda kutoka chupani*.

*Chura* [umbo] *anapanda* [usogezi + njia] *kutoka* [njia] *chupani* [chanzo].

112) *Mvulana na chura wametumbukia majini*.

*Mvulana na chura* [umbo] *wametumbukia* [usogezi + njia] *majini* [lengo].

Katika sentensi ya kwanza, njia husika ni njia ya chanzo huku sentensi ya pili ikiwa na njia ya lengo. Njia hizi zimefungamana na chanzo na lengo na kwa hivyo ni njia funge.

**4.2.1.2 Njia za Mwelekeo**

Katika aina hii ya njia, kirejelezi cha usogezi hakimo ndani ya njia. Hali hii inamaanisha kuwa si lazima umbo liwepo katika chanzo au lengo. Aina hii ya njia inatumika tu kueleza mwelekeo wa usogezi. Njia hizi hudhihirisha usogezi kuelekea kwa upande wa lengo au kutoka upande wa chanzo. Kwa mfano:

113) *Mbuzi anaelekea upande wa nyumba*.

*Mbuzi* [umbo] *anaelekea* [usogezi + njia] *upande wa nyumba* [mwelekeo].

Katika sentensi hii, umbo (mbuzi) halengi kufika katika nyumba. Tunatumia tu *nyumba* kueleza mwelekeo wa huo usogezi. Huenda mbuzi akabadilisha mwelekeo au akasimama njiani ama akapita *nyumba*. Wakati mwingine aina hii ya Njia haidhihirishi Msingi wa kurejelea usogezi husika. Kwa mfano:

114) *Wanyama walienda kaskazini kwa sababu ya kiangazi*.

*Wanyama* [umbo] *walienda* [usogezi + njia] *kaskazini* [lengo] *kwa sababu ya kiangazi*.

Njia iliyomo hapa inarejelea tu mwelekeo wa usogezi bila kutaja lengo mahususi. Kaskazini ni upande tu na si lengo mahususi katika usogezi huu.

#### 4.2.1.3 Njia za Mapitio


Njia za mapitio huhusisha njia ambamo kirejelezi cha usogezi kimo ndani ya njia hivi kwamba umbo lazima lipenyeze katikati ya kirejelezi hicho linaposonga. Kwa mfano:

115) *Wezi walipitia uani jana usiku*.

*Wezi* [umbo] *walipitia* [usogezi + njia] *uani* [msingi-pitwa] *jana usiku*.

Katika sentensi hii, umbo (wezi) linapita katikati ya kirejelezi (uani). Njia za mapitio hazionyeshi chanzo na lengo la kitendo sogezi.

a) Njia ya lengo b) Njia ya chanzo c) Njia ya mapitio



Mchoro 2: *Michoro ya aina mbalimbali za Njia. (Landau & Zukowski 2003:112)*

Njia ya usogezi huweza kuwa sahili au changamano. Njia sahili ni ile inayohusu kitendo sogezi kimoja tu kilicho na chanzo kimoja au msingi-pitwa mmoja au lengo moja tu. Slobin (1996) anaeleza kuwa njia huweza kurefushwa. Anaita njia iliyorefushwa safari. Ukweli ni kuwa vitendo sogezi, mara nyingi, huhusu njia changamano katika hali halisia. Njia changamano huhusisha maelezo ya vitendo sogezi kadha kwa kutumia njia moja. Katika njia changamano, kuna uwezekano wa kuwa na malengo kadha na matumizi ya vitenzi kadha vya usogezi. Kwa mfano:

116) *Mama alitoka kazini akapitia dukani kisha akaenda kwa mjomba na kuja nyumbani*.

*Mama* [umbo] *alitoka* [usogezi + njia] *kazini* [chanzo] *akapitia* [usogezi + njia] *dukani* [msingi-pitwa] *kisha akaenda* [usogezi + njia] *kwa mjomba* [lengo] *na kuja* [usogezi + njia] *nyumbani* [lengo].

Katika sentensi hii, njia ni ya *kutoka kazini hadi nyumbani*. Hata hivyo, kuna vijia vingine na malengo mengine ndani yake kama vile *akapitia dukani* na *akaenda kwa mjomba*. Mfano mwingine wa njia changamano huweza kupatikana katika maelezo ya matukio yanayodhihirika katika kurasa za 19, 20, 21 na 23 za kitabu cha Mayer (1969). Matukio ya kurasa hizo yanaweza kuelezwa ifuatavyo:

*117) Swara anamwinua mvulana kutoka juu ya jiwe kwa pembe zake. Anaanza kukimbia huku akiwa amembeba mvulana katikati ya pembe zake. Mbwa naye anakimbia. Wote wanaelekea katika mteremko. Swara anasimama ghafla na kumfanya mvulana kudondoka kutoka katikati ya pembe zake. Mvulana na mbwa wanaanguka na kutumbukia majini.*

Beavers, Levin & Tham (2009) wanaeleza kuwa lugha fulani hueleza maswala ya usogezi kwa kutegemea zile vipashio ilivyo navyo kimofolojia, kileksia na kisintaksia. Kwa hivyo, ni muhimu kubainisha vipashio ambavyo lugha ya Kiswahili hutumia kueleza kipengele cha njia ya usogezi. Mojawapo ya rasilmali ambayo Kiswahili hutumia kueleza njia ni vitenzi vya usogezi. Vilevile, hueleza kipengele hiki katika vipashio vingine tofauti na vitenzi vya usogezi. Vipashio hivi ndivyo nimeviita vifuatilizi na ambavyo ninatoa fasili yake katika sehemu ya 4.3.2. Ninavishughulikia vipashio vinavyoeleza njia katika Kiswahili hapa chini na kudhihirisha vinavyoeleza kipengele cha njia ya usogezi.

### 4.2.2 Njia katika Vitenzi

Lugha ya Kiswahili ina vitenzi kadha vinavyoleksisha kipengele cha njia katika mizizi yao pamoja na kipengele cha usogezi. Vitenzi hivi huleksisha usogezi na njia kwa pamoja katika mizizi yao. Kwa hivyo, kipengele cha njia ni sehemu ya maana ya kileksia ya vitenzi hivi. Kwa sababu hii, vitenzi hivi huitwa vitenzi vya njia na hutofautiana na vile vya namna kwa

kuwa havielezi namna katika mizizi yao. Kwa hivyo, vitenzi vya Njia huwa na muundo ufuatao wa kisemantiki:

Kitenzi [usogezi + njia]

Vitenzi vya njia vinapotumika katika sentensi, kipengele cha namna ya usogezi huelezwa katika vifuatilizi. Hata hivyo, mara nyingi kipengele cha namna huweza kuachwa bila kuelezwa lakini maana inayokusudiwa ikaeleweka.

Slobin (1996) anaonyesha kuwa lugha za mfumbatio-kifuatilizi hueleza njia kwa kina zaidi kuliko lugha za mfumbatio-tenzi. Anasema kuwa njia moja ya kudhihirisha tofauti hii ni kuhesabu idadi ya vitenzi vya usogezi vinavyojitokeza pekee au pamoja na kifuatilizi cha njia (kwa mfano *anguka* au *anguka chini*) na idadi ya vitenzi vya usogezi ambavyo vinafuatwa na kipashio kinachoeleza kuhusu njia (kwa mfano *anguka ndani ya mto*). Slobin anaviita vitenzi vya usogezi hivyo vya kwanza kama vitenzi viso-msingi huku aina ya pili akiviita vitenzi ongeza-msingi. Lugha ya Kiswahili pia hudhihirisha aina hizi za vitenzi vya usogezi. Kwa mfano:

118) *Mbwa ameanguka na chupa kichwani*.

*Mbwa* [umbo] *ameanguka* [usogezi + njia] *na chupa kichwani*.

Katika sentensi hii, msingi haujatajwa. Hata hivyo, msingi unatajwa waziwazi katika sentensi ifuatayo:

119) *Mbwa ameingiza kichwa chake <u>ndani ya chupa</u>*.

*Mbwa* [kisababishi] *ameingiza* [usogezi + njia] *kichwa chake* [umbo] *ndani ya chupa* [lengo].

Lugha ya Kiswahili ina vitenzi kadha vya usogezi ambavyo huleksisha njia katika mizizi yao. Vitenzi hivi hukifanya Kiswahili kuonyesha zile sifa za lugha za mfumbatio-tenzi. Capelle & Declerk (2005) wanaeleza kuwa vitenzi vya njia huweza kuelezwa upya kwa kutumia kitenzi kingine na KH, yaani KT kilicho na KH. Kulingana nao, hiki ni kigezo kizuri cha kupimia ikiwa kitenzi ni cha njia au la. Ninatumia kigezo hiki katika kuamua vitenzi vya usogezi vya njia katika Kiswahili. Kwa mfano:

120) *Mvulana <u>ametoka nyumbani</u>*.

121) *Mvulana ameenda nje ya nyumba*.

122) *Mvulana na mbwa waliibuka majini*.

123) *Mvulana na mbwa walitoka nje ya maji*.

Vitenzi vya usogezi katika lugha ya Kiswahili huweza kuonyesha njia za aina mbalimbali. Ninaziangazia njia hizo hapa chini.

#### 4.2.2.1 Vitenzi vya Njia funge

Nilivyoeleza hapo juu, Njia funge huweza kugawika kwa aina mbili- njia ya chanzo na njia ya lengo.

**a) Njia ya Chanzo**

Njia ya chanzo ni njia inayoanza katika chanzo cha usogezi. Kiswahili huwa na vitenzi vinavyoeleza njia ya chanzo cha kitendo sogezi husika. Kwa hivyo, vitenzi hivi hutumika tu wakati ambapo kitendo sogezi kinachorejelewa kinaanza katika chanzo. Vitenzi husika hapa ni kama vile *toka*, *ondoka* na *chomoka*. Kwa mfano:

*124) Panya ametoka shimoni.*

*Panya* [umbo] *ametoka* [usogezi + njia] *shimoni* [chanzo].

*125) Paka alichomoka chumbani alipofumaniwa akinywa maziwa.*

*Paka* [umbo] *alichomoka* [usogezi + njia + namna] *chumbani* [chanzo] *alipofumaniwa akinywa maziwa*.

126) *Papa ataondoka nchini leo jioni.*

*Papa* [umbo] *ataondoka* [usogezi + njia] *nchini* [chanzo] *leo jioni.*

Hata hivyo, si kila wakati ambapo vitenzi hivi hutokea pamoja na vipashio vinavyoeleza chanzo waziwazi. Kuna wakati ambapo vitenzi hivi vinapotumiwa chanzo hakitajwi lakini lengo linatajwa. Hata hivyo, nilivyotaja awali, hali hii huenda ikawa inatokana na mazoea ya watumiaji wa lugha kueleza lengo mara nyingi kuliko chanzo. Hali hii haivunji uhusiano uliopo kati ya njia inayoleksishwa na vitenzi hivi na chanzo cha kitendo sogezi. Kwa mfano:

*127) Mama ameondoka kwenda kwao jana jioni.*

*Mama* [umbo] *ameondoka* [usogezi + njia] *kwenda* [usogezi + njia] *kwao* [lengo] *jana jioni*.

*128)* *Babu atatoka kesho kuenda mjini.*

*Babu* [umbo] *atatoka* [usogezi + njia] *kuenda* [usogezi + njia] *mjini* [lengo] *kesho*.

129) *Mbwa amechomoka kuelekea mtoni.*

*Mbwa* [umbo] *amechomoka* [usogezi + njia + namna] *kuelekea* [usogezi + njia] *mtoni* [lengo] .

Katika mifano hii, chanzo hakitajwi lakini lengo linatajwa waziwazi- *kwao, mjini* na *mtoni*. Hata hivyo, bado tunaweza kupata kuelewa kuwa vitendo sogezi husika sharti viwe na chanzo.

**c) Njia ya Lengo**

Lugha ya Kiswahili huwa na vitenzi vinavyoeleza njia ya lengo. Vitenzi hivi ni pamoja na *ingia* na *fika*. Kwa mfano:

130) *Mwanafunzi amefika shuleni*.

*Mwanafunzi* [umbo] *amefika* [usogezi + njia] *shuleni* [lengo].

131) *Mkulima ameingia shimoni*.

*Mkulima* [umbo] *ameingia* [usogezi + njia] *shimoni* [lengo].

Vitenzi hivi hufungamana na lengo katika maelezo ya vitendo sogezi.

#### 4.2.2.2 Vitenzi vya Njia ya Mapitio

Vipo vitenzi vinavyoonyesha kuwa umbo linasonga kupitia msingi fulani. Vitenzi hivi ni kama vile pitia na vuka. Kwa mfano:

132) *Mvulana na mbwa wamevuka mto*.

*Mvulana na mbwa* [umbo] *wamevuka* [usogezi + njia] *mto* [msingi].

Sentensi hii inamaanisha kuwa mvulana na mbwa wamesonga ndani ya mto kutoka upande mmoja hadi mwingine.

#### 4.2.2.3 Vitenzi vya njia ya Mwelekeo

Kiswahili huwa na vitenzi vingine vinavyoeleza njia za mwelekeo. Kitenzi kinachuhusika hapa mara nyingi ni *elekea*. Kwa mfano:

*133) Mifugo wanaelekea shambani.*

*Mifugo* [umbo] *wanaelekea* [usogezi + njia] *shambani* [msingi].

Sentensi hii inamaanisha kuwa usogezi unatendeka kuelekea upande wa shamba lakini si lazima mifugo wawe wanalenga kuingia shambani. Kwa hivyo, hapa *shamba* si lengo mahususi bali ni msingi unaotumiwa tu kurejelea mwelekeo wa usogezi.

### 4.2.3 Njia katika Kifuatilizi

Talmy (1991:486) anaifasili kifuatilizi kama kipashio cha kisarufi kilicho tofauti na yambwa na kilicho na uhusiano wa kidada na kitenzi. Tunaweza kutumia kielelezo kifuatacho kueleza fasili hii ya Talmy kuhusu kifuatilizi.

X ni kifuatilizi, na X $\neq$ KN

Katika lugha ya Kiswahili, kimsingi, kifuatilizi huja baada ya kitenzi cha usogezi katika sintaksia.

#### 4.2.3.1 Njia katika Kihusishi au KH

Kiswahili vilevile hueleza kipengele cha njia kwa kutumia kirai husishi (KH). KH husika hapa hujengwa kwa vihusishi kama vile *hadi, kuanzia, kutoka, mpaka* na *katika*. KH huweza kueleza aina zote tatu za njia ilivyo na vitenzi vya usogezi vya njia.

##### 4.2.3.1.1 Njia funge

Kipengele cha njia huweza kuelezwa katika KH katika Kiswahili sanifu. Vihusishi vinavyojenga KH husika ni vile vya kiasilia kama vile *hadi*, *mpaka* na vilivyoundwa kutokana na vitenzi kama vile *kutoka* na *kuanzia*. Kwa mfano:

134) *Mzinga wa nyuki umeanguka <u>kutoka juu ya mti</u>.*

*Mzinga wa nyuki* [umbo] *umeanguka* [usogezi + njia] *kutoka juu ya mti* [ njia ya chanzo].

KH *kutoka juu ya mti* kinaeleza kuhusu njia funge kwa kuwa kinataja kuhusu njia inayofungamana na chanzo. Ninatoa mfano zaidi hapa chini.

135) *Wanariadha wamekimbia kuanzia Kapkatet hadi Nandi*.

*Wanariadha* [umbo] *wamekimbia* [usogezi + namna] *kuanzia Kapkatet* [njia ya chanzo] *hadi Nandi* [njia ya lengo].

Katika sentensi hii, KH *kuanzia Kapsabet* kinarejelea njia inayofungamana na chanzo huku KH *hadi Nandi* kikirejelea njia inayofungamana na lengo.

#### 4.2.3.1.2 Njia za Mwelekeo

Njia za mwelekeo vilevile huweza kuelezwa kwa kutumia KH katika Kiswahili sanifu. KH husika hapa ni kama vile *kando ya, karibu na, juu ya, nyuma ya* na *chini ya*. Kwa mfano:

136) *Mwanafunzi anatembea karibu na bweni*.

137) *Ndege wanapaa juu ya mlima*.

Sentensi hizi zina virai husishi vinavyorejelea njia za mwelekeo kwa kuwa *bweni* na *mlima* zinatumiwa tu kueleza mwelekeo wa usogezi na huenda zisiwe lengo la usogezi huo.

#### 4.2.3.1.3 Njia za Mapitio

Nilivyoeleza hapo juu, njia za mapitio huhusisha umbo kupita katikati ya kitu kingine, yaani linapenyeza katikati ya kitu kingine likiwa njiani kuelekea katika lengo lake. Kiswahili sanifu huweza kueleza njia za mapitio kwa kutumia KH. Kwa mfano:

138) *Mwizi alipita katikati ya majengo mawili*.

### 4.3 Mifumo ya Urejelezi na Njia za Vitendo sogezi

Mifumo ya urejelezi iliyopendekezwa na Levinson (2004) hutumiwa kuchunguza nafasi katika lugha, kwa mfano, alivyofanya Ngina (2015) katika lugha ya Kikamba. Hata hivyo, mifumo hii pia huweza kutumiwa katika kueleza njia za vitendo sogezi. Noonan (2003) anaeleza kuwa mwelekeo wa usogezi huweza kuelezwa katika mifumo yote mitatu japo si

lazima lugha moja itumie mifumo yote katika maelezo yake ya njia ya usogezi. Lugha ya Kiswahili pia hutumia mifumo hii ya urejelezi kueleza njia ya vitendo sogezi vyake. Aina za njia ambazo nimezitaja juu huweza kuhusishwa na angalau mfumo mmoja wa urejelezi. Ninadhihirisha uhusiano huu hapa chini.

### 4.3.1 Mfumo wa Urejelezi Sahili

Mfumo wa urejelezi sahili huweza kutumiwa kueleza usogezi unaoelekea katika chanzo mahususi au lengo mahususi. Hapa lengo au chanzo husika ndio unadhihirisha mwelekeo wa usogezi husika. Kwa hivyo, njia inaweza kuwa kuelekea lengo au kutoka chanzo ama ikapita msingi-pitwa. Kilicho muhimu hapa ni kuwa mwelekeo wa usogezi huelezwa kwa kuzingatia kipengele fulani cha msingi. Kwa mfano:

139) *Mkulima ameingia shambani*.

140) *Chura aliondoka ndani ya chupa*.

141) *Siafu wanapitia nyufa katika ukuta*.

Tunavyoona katika mifano ya hapo juu, njia funge huhusiana na mfumo huu wa urejelezi. Tunaeleza njia ya usogezi kwa kurejelea mwelekeo wa umbo kutoka chanzo au kuelekea lengo.

### 4.3.2 Mfumo wa Urejelezi Husishi

Mfumo huu hueleza mwelekeo wa usogezi kwa kuzingatia alipo msemaji. Kwa hivyo, ninalishughulikia swala la usonde ndani ya mfumo huu. Kiswahili kina vitenzi vya usonde katika leksikoni yake. Kulingana na Talmy (2000), vitenzi vya usogezi vya usonde ni aina ya vitenzi vinavyoeleza njia ya usogezi iliyo na njia na msingi maalumu. Anaeleza kuwa kipengele cha kiusonde cha njia hueleza mwelekeo wa kuenda kwa msemaji. Vitenzi hivyo ni *-enda, -ja, njoo,* na *-rudi*. Mara nyingi vitenzi hivi vikitumiwa kueleza kitendo sogezi, usogezi huwa unaelekea au kutoka alipo msemaji. Kwa mfano:

142) *Njoo haraka*.

Katika sentensi hii, mlengwa atasonga kutoka aliko akielekea kwa msemaji kwa kuwa kitenzi hiki kinabeba maana ya njia ya kuelekea kwa msemaji. Sentensi hii vilevile inaweza kuandikwa upya kwa kutumia kitenzi *-ja*.

143) *Kuja haraka*.

Njia ya usogezi unaorejelewa hapa ni kuelekea kwa msemaji. Kwa hivyo, katika sentensi hizi mbili, njia ya usogezi inaamuliwa na matumizi ya vitenzi hivi na kuwa msingi wa kurejelea mwelekeo huo ni msemaji. Nakazawa (keshatajwa) anaeleza kuwa kitenzi kuja (na bila shaka njoo) huwa na maana ya kileksia ya "songa kuelekea mahali sawia na alipo msemaji." Kitenzi *-rudi* pia huonyesha njia ya kuelekea kwa msemaji hasa kisipofuatwa na neno jingine la kuonyesha mwelekeo tofauti. Kwa mfano:

144) *Mwanangu rudi*.

Hata hivyo, *-rudi* pia huweza kuwa na maana ya kusonga kutoka aliko msemaji hasa kinapofuatwa neno linalotaja lengo tofauti na alipo msemaji. Kwa mfano:

145) *Mwanangu rudi shuleni*.

146) *Nimekueleza urudi ulikotoka*.

Sentensi hizi zinaonyesha usogezi unaoelekea kwingine kutoka alipo msemaji.

Vitenzi hivi vya usonde vinaweza kutumiwa peke yao bila kuongeza maneno mengine ya usonde, jinsi nimedhihirisha hapo juu, au vikatumiwa na maneno mengine ya usonde. Kwa mfano:

*147) Njoo hapa haraka.*

148) *Kuja huku haraka*.

Kitenzi cha usogezi *-enda* kinaweza kuonyesha njia ya kutoka kwa msemaji. Nakazawa (2007) anaongezea kuwa maana ya kileksia ya kitenzi *-enda* ni "songa kuelekea mahali ambapo si alipo msemaji." Hata hivyo, ni vyema kuongeza kuwa huko kusonga kunaazia alipo msemaji. Kwa mfano:

149) *Mama ameenda sokoni leo*.

Msemaji wa sentensi hii anachukuliwa kuwapo mahali ambapo mama alianzia safari yake kuelekea sokoni. Kwa hivyo, msingi wa kurejelea mwelekeo wa usogezi wa mama ni msemaji. Kwamba mama alitoka mahali alipo msemaji na kuelekea sokoni asipokuwapo msemaji.

Nakazawa (keshatajwa) anaeleza kuwa si kila mara vitenzi hivi vinapotumiwa basi vinarejelea usogezi kwenda alipo msemaji. Madai yake yanaoana na ya Botne (2005) ambaye pia alivishughulikia vitenzo sogezi vya usonde katika Kichandali. Hali hii vilevile inadhihirika katika Kiswahili sanifu. Kwa mfano, kitenzi kuja kinaweza kutumika kurejelea usogezi unaoelekea kwa msikilizaji inavyoonekana katika sentensi hii ya hapa chini.

150) *Daktari atakuja kukuona kesho*.

Usogezi unaotendeka katika sentensi hii hauelekei kwa msemaji bali alipo msikilizaji. Sentensi hii bado itakuwa na mantiki hata kama msemaji hayupo katika sehemu moja na msemewa. Kwa hivyo, inaonekena wazi kuwa hata msemewa pia anaweza kuchangia Msingi wa njia katika maana ya vitenzi vya usogezi vya usonde katika Kiswahili. Vilevile, msemaji anaweza kutumia -*enda* hata kama hayupo pamoja na msemewa. Kwa mfano:

*151) Utaenda nikifika nyumbani.*

Katika sentensi hii, tunaweza kuchukulia kuwa msemewa yupo nyumbani na ataanza kusonga kutoka hapo wakati msemaji atakapofika hapo. Kwa hivyo, msemaji anapotumia kitenzi -*enda*, anazingatia mahali atakapokuwa huo wakati ujao bali si alipo wakati wa kuisema sentensi hii.

Vilevile, matumizi ya viambishi vya nafsi pamoja katika vitenzi vilivyo katika kauli ya kutendea hueleza mwelekeo wa usogezi. Kwa hivyo, tukitumia vitenzi hivi katika kauli ya kutendea na viambishi vya nafsi, tunaweza kueleza mwelekeo wa usogezi kwa kumtegemea msemaji, msemewa au mrejelewa. Kwa mfano:

*152) Ndovu ananijia.*

*153) Ndovu anakujia.*

*154) Ndovu anamjia.*

Sentensi ya 152 inarejelea usogezi kwa kumrejelea msemaji huku ya 153 ikirejelea usogezi kwa kuzingatia alipo msemewa. Sentensi ya 154 inaeleza mwelekeo wa usogezi kwa kutegemea mrejelewa mwingine tofauti na msemaji na msemewa. Kwa hivyo, inadhihirika kuwa kuambisha viambishi vya nafsi na vya kauli ya kutendea katika vitenzi hivi kunabadili msingi wao wa kurejelea mwelekeo wa usogezi. Kwa hivyo, viambishi hivi huweza kuathiri mwelekeo wa usogezi hasa kwa vitenzi hivi vinavyochukuliwa kuwa vya kiusonde.

Njia ya usogezi inayohusiana na mfumo huu wa urejelezi ni njia funge. Vitenzi vya njia vinavyohusika hapa hufungamana na vyanzo na malengo maalumu.

### 4.3.3 Mfumo wa Urejelezi Halisi

Mfumo huu wa urejelezi huweza kutumiwa kurejelea usogezi unaoelekea katika malengo yasiyo mahususi na ambayo ni pande za kijiografia. Kwa hivyo, usogezi unaoelezwa hapa ni usiokuwa funge kwa kuwa lengo si mahususi. Upande wa mashariki, kwa mfano, si lengo mahususi na kwamba hatuwezi kujua umbo litasonga kuelekea huku hadi wapi na lini. Kwa mfano:

155) *Ndege ya abiria ilipaa kuelekea kaskazini*.

Aina ya njia inayohusiana na mfumo huu wa urejelezi ni njia za mwelekeo. Tunaeleza tu mwelekeo wa usogezi lakini kirejelezi cha mwelekeo huo si lazima liwe lengo au chanzo cha usogezi husika.

## 4.4 Muhtasari

Nimeshughulikia kipengele cha njia katika sura hii. Nimedhihirisha vipashio mbalimbali ambavyo vinatumiwa katika lugha ya Kiswahili kueleza kipengele hiki. Pia, nimebainisha aina tatu za njia zinazojitokeza katika Kiswahili. Nimemailiza kwa kuonyesha uhusiano uliopo kati ya kipengele cha njia na mifumo ya usogezi iliyoelezwa na Levinson (2004). Katika sura inayofuatia nitahitimisha tasnifu hii kwa kuonyesha matokeo ya utafiti na kutoa mapendekezo mbalimbali.

SURA YA TANO

# 5.0 MATOKEO YA UTAFITI NA HITIMISHO

## 5.1 Utangulizi

Utafiti huu ulilenga kubainisha uainisho unaofaa Kiswahili kuhusiana na vitendo sogezi. Vilevile, utafiti huu ulinuiwa kuonyesha vipashio vinavyotumiwa katika Kisawhili sanifu kueleza vipengele mbalimbali vya vitendo sogezi. Katika sura zilizotangulia, nimeshughulikia vipashio vinavyotumika katika Kiswahili kueleza vipengele mbalimbali vya usogezi. Kwa jumla, nimeangazia maelezo ya vipengele vitano vya ndani (umbo, njia, chanzo, msingi-pitwa na lengo) na viwili vya nje (kisababishi na namna). Kwa hivyo, nimeonyesha wazi kipengele kipi cha kileksia au kisintaksia kinachoeleza kipengele kipi cha kisemantiki cha vitendo sogezi. Hivyo basi, katika sura hii, ninawasilisha matokeo ya utafiti huu na kutoa hitimisho.

## 5.2 Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu ulikuwa na malengo matatu. Nimepata matokeo mbalimbali yanayohusiana na malengo hayo katika utafiti huu. Jedwali 1 linatoa muhtasari wa vipashio vinavyotumiwa kueleza vipengele vya kisemantiki vya vitendo sogezi.

| | Kipengele cha Usogezi | Kipashio cha Maelezo |
|---|---|---|
| | Umbo | a) Nomino na Kirai Nomino |
| | Chanzo | a) Kirai husishi<br>b) Kielezi na Kirai elezi<br>c) Kishazi kitegemezi |
| | Msingi-pitwa | a) Nomino na Kirai nomio |
| | Lengo | a) Nomino<br>b) Kielezi na Kirai elezi<br>c) Kishazi kitegemezi |
| | Njia | a) Vitenzi vya Njia<br>b) Kirai husishi |
| | Namna | a) Vitenzi vya Namna<br>b) Vielezi na Kirai elezi<br>c) Kirai husishi<br>d) Tashibihi |

| | | |
|---|---|---|
| | | e) Viigizi |
| | Kisababishi | a) Nomino na Kirai Nomino |

*Jedwali 1: Muhtasari wa vipashio vinavyoeleza vipengele vya Usogezi*

Hata hivyo, ili kujua kwa umahususi uainisho unaokifaa Kiswahili kuhusiana na vitendo sogezi, sharti tuzingatie maelezo ya kipengele cha njia. Vitenzi tulivyovipata katika data yetu vinaonyesha miundo ifuatayo ya kisemantiki:

a) Kitenzi [usogezi + njia] – vitenzi ishirini na mbili (21)

Vitenzi hivi ni vifuatavyo: *rudi, njoo, kuja, enda, panda, shuka, tumbukia, ibuka, toka, ondoka, ingia, anguka, pita, vuka, elekea, piku, fika, andama, fukuza, sindikiza* na *zunguka.*

b) Kitenzi [usogezi + namna] – vitenzi saba (09)

Vitenzi hivi ni vifuatavyo: *paa, elea, teleza, kimbia, tembea, ruka, ogelea, tiririka* na *bingiria.*

c) Kitenzi [usogezi + njia + namna] – vitenzi vitatu (03)

Vitenzi hivi ni vifuatavyo: *chomoka, toma* na *kurupuka*.

Kwa hivyo, kati ya vitenzi vya usogezi thelathini na tatu (33) tulivyoviangazia katika utafiti huu, vitenzi vya njia ndivyo vingi zaidi vikifuatwa na vya namna kisha vya mchanganyiko.

Vilevile, nimebainisha kuwa upo uhusiano wazi kati ya mifumo ya urejelezi na njia ya usogezi katika lugha ya Kiswahili. Tunaona kuwa aina zote tatu za njia zinaweza kuelezeka katika angalau mojawapo ya mifumo ya urejelezi. Vilevile, nimebainisha kuwa uambishaji wa viambishi vya kauli ya kufanyia na viambishi vya nafsi huweza kubadilisha mwelekeo wa usogezi au msingi unaotumiwa kurejelea mwelekeo wa usogezi husika.

Kwa kuwa mada ya vitendo sogezi haijafanyiwa utafiti mwingi katika Kiswahili, ninapendekeza utafiti zaidi kufanywa kuhusu mada zinazohusiana na vitendo sogezi. Mada hizi zinajumuisha namna watoto wanavyojifunza kueleza vipengele mbalimbali

vya vitendo sogezi, namna magonjwa ya ubongo yanaweza kuathiri uwezo wa mtumiaji wa Kiswahili kueleza vipengele vya vitendo sogezi na ulinganishi na ulinganuzi wa maelezo ya vitendo sogezi katika Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu au za jamii tofauti.

### 5.3 Hitimisho

Ninahitimisha kwa kusema kuwa lugha ya Kiswahili kina vipashio vya kueleza vipengele vyote vya vitendo sogezi. Vipengele hivyo vinaweza kuwa neno moja ua utungo wa maneno kadha.

Kwa kuzingatia sifa alizozitoa Talmy (1985, 2000), Slobin (2000) na Zlatev & Yangklang (2004) kuhusu lugha za mfumbatio-tenzi na mfumbatio-kifuatilizi, Kiswahili ni lugha ya mfumbatio-tenzi. Kina vitenzi vingi vinavyoeleza njia kuliko vile vinavyoeleza namna. Pia, idadi kubwa ya vipashio vinavyoeleza namna katika Kiswahili ni thibitisho kuwa Kiswahili hupendelea zaidi kueleza namna ya vitendo sogezi katika vifuatilizi badala ya vitenzi. Kwa hivyo, mfumo unaopendelewa na Kiswahili ni wa kueleza njia katika mizizi ya vitenzi vya usogezi huku namna ikielezwa katika vifuatilizi.

Mwisho, njia na mwelekeo wa vitendo sogezi huweza kuelezeka katika mifumo ya urejelezi. Kwa hivyo, mifumo ya urejelezi haihusu nafasi pekee bali pia vitendo sogezi katika lugha ya Kiswahili.

**MAREJELEO**

Allwood, J. & Gardenfors, P.(Wah.). (1999). *Cognitive Semantics: Meaning and Cognition*. Amsterdam: John Benjamins Publishing Company.

Ameka, F.K & Essegbey, J. (2013). Serializing Languages: Satellite-framed, Verb-framed or neither. *Ghana Journal of Linguistics 2*,1: 19-38.

Antunano, I.I .( 2009). Path Salience in Motion Events. Katika Guo, J. et al. (Wah.) *Crosslinguistic Approaches to the Psychology of Language: Research in the Tradition of Dan Isaac Slobin* (uk. 403-414). New York: Taylor & Francis Group.

Beavers, J., Levin, B & Tham, W. (2009). Motion expressions revisited. *Journal of Linguistics: 1-47*. Cambridge: Cambridge University Press.

Botne, R. (2005). Cognitive Schemas and Motion Verbs: Coming and Going in Chandali (Eastern Bantu). *Cognitive Linguistics 16, 1*: 43-80.

Capelle, B. & Declerk, R. (2005) Spatial amd temporal boundedness in English Motion events. *Journal of Pragmatics 37*: 889-917.

Chen, L. & Guo, J. (2009). Motion Events in Chinese novels: Evidence for an equipollently-framed language. *Journal of Pragmatics* 41: 1749-1766.

Evans, V. & Green, M. (2006). *Cognitive Linguistics: An Introduction*. Edinburgh: Edinburgh University Press.

Fortis, J.M. (2010). The Typology of Motion Events in Space in Language. *Leipzig Summer School*: 1-34.

Filipovic', L. (2007). *Talking about Motion: A Cross-linguistic Investigation of Lexicalization patterns.* Amsterdam: John Benjamin Publishing Company.

Gardenfors, P. (1999). Some Tenets of Cognitive Semantics. Katika Allwood, J. & Gardenfors, P. (Wah.). *Cognitive Semantics: Meaning and Cognition* (uk. 19-36) Amsterdam. John Benjamin Publishing Company.

Geeraerts, D. (2009). *Theories of Lexical Semantics*. Oxford: Oxford Scholarship Online.

Genaari, S.P., Sloman, S.A., Malt, B.C. & Fitch, W.T. (2001). Motion Events in Language and Cognition. *Cognition 83*, 49-79.

Goschler, J. & Stefanowitsch, A. (2013). *Variation and Change in the Encoding of Motion Events*. Amsterdam: John Benjamin Publishing Company.

Hoffman, D. (2011). Description of Motion and Travel in Jaminjung and Kriol. (PhD Thesis at University of Manchester).

Jackendoff, R. (1983). *Semantics and Cognition*. Cambridge: MIT Press.

Jerono, P. (2017, May). Typology of Motion in Tugen. Makala iliyowasilishwa katika Kongamano la 13 ya Nilo-Sahara, Addis.

Lakusta, L.M. (2005). Source and Goal Asymetry in Non-linguistic Motion Event Representations. (PhD Dessertation at The John Hopkins University).

Lakusta, L., Wagner, L., O'Hearn, K. & Landau, B. (2007) Conceptual Foundations of Spatial Language: Evidence for a Goal Bias in Infants. *Language Learning and Development, 3(3)*: 179-197.

Landau, B. & Zukowski, A. (2003) Objects, Motions, and Paths: Spatial Language in Children With Williams Syndrome. *Developmental Neuropsychology 23(1-2)*: 105-137, DOI: 10.1080/87565641.2003.9651889

Langacker, R.W. (1987). *Foundation of Cognitive grammar*: *Theoretical Perspectives*: Stanford: Stanford University Press.

Levin, B. (1993). *English Verb Classes and Alternations: A Preliminary Investigation*. Chicago: University of Chicago Press.

Levinson, S.C. (2004) *Space in Language and Cognition: Explorations in Cognitive Diversity*. Cambridge: Cambridge University Press.

Massamba, D.P.B., Kihore, Y.M. & Hokororo, J.I. (2001). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salam. TUKI.

Matlock, T., Holmes, K.J., Srinivasan, M. & Michael, R. (2011). Even Abstract Motion Influences the Understanding of Time. *Metaphor and Symbol* 26: 260-271. Psychology Press: Taylor & Francis Group.

Mayer, M. (1969). *Frog, Where Are You: Sequel to a Boy, a Dog and a Frog*. New York: Dial Books for Young Readers.

Mgullu, R.S. (1999). *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki*, *Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Mohamed, M.A. (2001). *Modern Swahili Grammar*. Nairobi: East Africa Educational Publishers Ltd.

Myachina, E.N. (1981). *The Swahili Language*. London: Routledge & Kegan Paul Ltd.

Nakazawa, T. (2007). A Typology of The Ground Deictic Motion Verbs As Path-conflating Verbs: The Speaker, the Addressee and Beyond. *Poznan Studies in Contemporary Linguistics* 43-2. Poznan: Adam Mickiewicz University. Makala iliyowasilishwa katika Warsha kuhusu Miundo ya Matukio Leipzig, Ujerumani.

Nam, S (2004) Goal and Source: Assymetry in their Syntax and Semantics.

Ngina, F.K. (2015). A Semantic Analysis of Kikamba Spatial expressions using the Cognitive Semantics Theory. (M.A Thesis at University of Nairobi).

Noonan, M. (2003). Motion Events in Chantyal. Crossasia-repository.ub.uni-heidelberg.de/191/1/Chantyal_Motion_Events.pdf

Schaefer, R.P, & Gaines, R. (1997). Toward a Typology of Directional Motion for African Languages. *Studies in African Linguistics* 26, 2: 193-220.

Slobin, D.I. (1996) Two Ways to Travel: Verbs of Motion in English and Spanish. Katika Shibatani, M. & Thompson, S.A (Wah.). *Grammatical Constructions: Their form and Meaning* (uk. 195-220). New York: Oxford University Press.

Slobin, I.D. (2000). Verbalised Events. A Dynamic Approach to Linguistic Relativity and Determinism. Katika Niemeier, S. & Dirven, D. (Wah) *Evidence of Linguistic Relativity* (uk.107-138). Amsterdam: John Benjamins Publishing Company.

Slobin, D.I. (2004). The Many ways to search for a frog: Linguistic typology and the expression of motion events. Katika Stromqvist, S. & Verhoeven, L. (Wah.) *Relating Events in Narratives: Typological and Contextual Perspectives* (uk. 219-257). London: Lawrence Erbaum Associates.

Slobin, D.I. (2005). Linguistic Representation of Events: What is Signifier and What is Signified. Katika Maeder, C., Fischer, O. & Herlofsky, W.J. (Wah.) *Iconicity Inside Out: Iconicity in Language and Literature* (uk. 307-322). Amsterdam: John Benjamins Publishing Company.

Talmy, G. (1972). Semantic Structures in English and Atsugewi. (Doctoral dissertation, University of California at Berkeley).

Talmy, L. (1975). Figure and Ground in Complex Sentences. *Proceedings of the First Annual Meeting of Berkeley Linguistics Society*: 419-430.

Talmy, L. (1985). Lexicalization Patterns: Semantic Structure in lexical forms. Katika Shopen, T. (Mh.). *Language typology and syntactic description*. Vol.III: Grammatical Categories and the lexicon (uk. 57-149 ). Cambridge: Cambridge University Press.

Talmy, L .(1991). Path to Realization: A typology of Event Conflation. Katika Sutton, L.A, Johnson, C. & Shields, R.B. (Wah.). *Proceedings of the Seventeenth Annual Meeting of the Berkeley Linguistics Society 480-519*. Berkeley Linguistics Society, Berkeley.

Talmy, L. (2000). *Toward Cognitive Semantics*. Massachusetts: MIT Press.

Papafragou, A, Massey, C. & Gleitman, L. (2002). Shake, rattle, 'n' roll: the representation of motion in Language and Cognition. *Cognition 84*: 189-219

Papafragou, A., Massey, C. & Gleitman, L. (2006). When English Proposes what Greek presupposes: The cross-linguistic encoding of Motion events. *Cognition 98,3*: 75-87.

Ungerer, F & Schimid, H.J. (2006). *Introduction to Cognitive Linguistics*. London: Taylor and Francis Group.

Zwarts, J. (2004, October). Events shape: Paths in the Semantics of verbs. Makala iliyowasilishwa katika warsha ya "Geometrical structure in Events Concepts": Chuo Kikuu cha Konstanz.

Zlatev, J & Yangklang, K. (2004). A Third way to travel: The Place of Tahi in Motion-event typology. Katika Stromqvist, S. & Verhoeven, L. (Wah.) *Relating Events in Narratives: Typological and Contextual Perspectives* (uk. 219-257). London: Lawrence Erbaum Associates.